Jarida la
# UQAB

TOLEO MAALUM



*Toleo 32 - Muharram 1440 H / Septemba 2019 Miladi*



# VIJANA WAISLAMU

## Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi

uqab.or.ke uqab_htk UQAB-Magazine-1911964012162253

# Changamoto za Kiulimwengu Kwa Utambulisho wa Kiislamu wa Vijana Waislamu

**Hotuba ya Kwanza Katika Kongamano: ‘Vijana Waislamu …Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi’**

Dada zangu wapendwa, Mwenyezi Mungu (swt) asema katika Surah Al-Anbiyah,

بَلْ نَقْذِفُ بِٱلْحَقِّ عَلَى ٱلْبَٰطِلِ فَيَدْمَغُهُۥ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌۚ وَلَكُمُ ٱلْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ

“Bali tunaitupa haki juu ya batili ikaivunja na mara ikatoweka. Na ole wenu kwa mnayo yazua.” [Al-Anbiyah: 18]

Katika ayah hii ya Qur’an, Mwenyezi Mungu Mwingi wa nguvu, Mwingi wa hekma atuambia kuwa kutakuweko na mvutano baina ya Haki na Batili kuanzia mwanzo hadi mwisho. Leo dada zangu, hakuna shaka kuwa kuna mvutano wa kimfumo wa kiulimwengu unaotekelezwa na mashirika ya kisekula ya kimataifa na serikali za Kimagharibi wakisaidiwa na serikali zisizo kuwa za Kiislamu katika ulimwengu wa Waislamu dhidi ya Uislamu. Moja ya malengo makuu ya mvutano huu ni kuwavuna vijana Waislamu katika mfumo na nidhamu huru ya kimaisha. Hili lilidhihirishwa waziwazi katika barua iliyoandikwa mnamo 2004 na Sir Andrew Turnbull, aliyekuwa Waziri wa Uingereza katika Afisi ya Kigeni ya Jumuiya ya Madola ambapo alitoa wito wa kuwepo kwa mpango wa kuvuna “nyoyo na akili” za vijana Waislamu. Lengo moja kwa moja la ajenda hii ni – kuzuia mwamko wa Uislamu kiulimwengu na kusimama kwake kama nidhamu ya kisiasa katika biladi za Waislamu ambao utapambana na utawala na kutishia maslahi ya kisiasa na kiuchumi ya serikali za Kimagharibi kimataifa.

Mwaka huu, mnamo 27 Machi 2016, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-Moon alizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Jordan, Amman, na kusema yafuatayo, “Katika miaka yangu kumi kama Katibu Mkuu, nimeufanya ushirikiano na vijana kuwa kipaumbele kwa mfumo mzima wa Umoja wa Mataifa. Idadi isiyo na kifani ya miradi na mipango ya Umoja wa Mataifa kwa sasa imeelekezwa kwa vijana wa kiume na wa kike. Vijana sio tu ni viongozi wa kesho; ni viongozi wa leo. Na nyinyi ni sehemu ya kizazi kikubwa kabisa cha vijana katika historia. Katika nchi nyingi za Kimagharibi, umri wastani ni juu ya miaka 40. Lakini katika ulimwengu mzima wa Kiarabu, umri wastani ni chini ya miaka 30. Hapa nchini Jordan, ni miaka 22. Hivyo ndivyo wasomi wa hesabu ya watu wanavyouita ‘haiba ya ujana’”

Hakika, asilimia 60 ya idadi ya Waarabu pekee, sawia na watu milioni 200 wako chini ya umri wa miaka 25. Idadi hii kubwa ya vijana Waislamu wanao wakilisha nishati, nguvu na mwelekeo wa Ummah huu, ikiongezewa na ongezeko la vijana Waislamu kushikamana na Uislamu, Mashariki na Magharibi, imewafanya kuwa walengwa wakuu wa serikali za kisekula na taasisi za kimataifa ambao wameunda mkakati kabambe unaolenga kujenga fikra, miondoko, matamanio na utiifu wao kwa maadili huru ya Kimagharibi na kuwaweka mbali kutokana na Dini yao.

Mnamo 2004, shirika la RAND, mdadisi mkuu wa sera ya kiulimwengu linalo fadhiliwa na serikali ya Amerika lilichapisha ripoti kwa anwani, “Vipi Magharibi Itaweza Kupigia debe Marekebisho ya Uislamu.” Ilisema kuwa ‘wanamambo leo’ wanaounga mkono marekebisho ya Uislamu kwa misingi huru ya Kimagharibi wanapaswa kushajiishwa kuandika kwa ajili ya vijana na maoni yao yanapaswa kupenyezwa katika mtaala wa elimu ya Kiislamu. Ilisema kuwa usekula unapaswa kufanywa kama chaguo dhidi ya thaqafa kwa vijana wa Kiislamu ambao hawaja athirika na kwamba utambulishaji wa historia ya nyuma na isiokuwa ya Kiislamu unapaswa kurahisishwa kupitia vyombo vya habari na mitaala ya nchi husika; na ilipigia debe utumaji jumbe kwa vijana dhidi ya wale wanao pigia debe sheria na utawala wa Kiislamu. Shirika la RAND linalo husishwa na mtandao wa Atlas, unaojumuisha zaidi ya mashirika 400 tofauti tofauti katika zaidi ya nchi 80! Iko wazi kuona jinsi gani shirika moja pekee laweza kuwafikia mamilioni ya vijana Waislamu. Hakika, ufikiaji na ushawishi wake ni mpana mno na wa aina tofauti tofauti kiasi ya kuwa wengi wetu au watoto wetu tayari washakuwa katika mawasiliano na miradi yao bila ya hata kujua.

Kwa muongo mmoja na zaidi uliopita, taasisi na serikali za kimataifa kote ulimwenguni zimejifunga na mkakati kwa ajili ya vijana Waislamu, ukiwakilishwa kupitia malengo ya RAND. UNESCO kwa mfano, shirika la Umoja wa Mataifa linalo jumuisha nchi wanachama 195 ambalo linapigia debe ushirikiano miongoni mwa mataifa kupitia elimu na thaqafa, lilizindua mpango wa kiulimwengu mwaka jana wa kutumia vijana kupigana dhidi ya jumbe za mtandaoni “zenye misimamo mikali”. Mnamo Novemba mwaka jana, pia pamoja na Wizara ya Kigeni ya Amerika ilikuwa mwenyeji wa tukio la kiwango cha juu lililo hamasisha mawaziri wa elimu wa nchi wanachama wake kutumia elimu katika mikakati ya kitaifa ili kutatua vyanzo vya misimamo mikali kwa vijana. Cha kufurahisha, Irina Bokoya, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, alipokuwa akizungumza kuhusu mpango huu alisema, “Mojawapo ya dori zetu kubwa kabisa, tulizo nazo, ni kuzibadilisha mujtama…” Kuzibadilisha mujtama kuwa nini lau utauliza. Kwa kweli, Julian Huxley, kinara wa kwanza wa UNESCO alisema, “Kazi iliyo mbele ya UNESCO … ni kusaidia kuibuka kwa thaqafa moja iliyo na filosofia yake na fikra zake na lengo lake pana.” Thaqafa hii moja, dada zangu, ni ile iliyo jengwa juu ya msingi wa maadili huru ya kisekula ya Kimagharibi – itikadi kama vile watu kuwa na uhuru wa kijinsia wa kuwa na uhusiano wowote waupendao;

*Endelea Uk..3*

itikadi kuwa demokrasia ambapo watu hutunga sheria, na sio Mwenyezi Mungu ndio inapaswa kupangilia siasa za dola; ambapo wanaume na wanawake wanapaswa kuwa na haki na majukumu sawa kwa mujibu wa usawa wa kijinsia; itikadi kuwa dini isiathiri mambo ya mujtama, na kwamba utiifu unapaswa kuwa kwa nchi ya mtu kuliko katika Dini yake. Hakika, mnamo 2011, kufuatia mapinduzi ya Kiarabu, UNESCO ilitangaza ruwaza yake ya kusaidia mustakbali wa kisekula na kidemokrasia wa dola za eneo hilo, kwa kutumia vijana wa Kiarabu kama kiungo muhimu cha mpango huu. Amali zake zilizo tajwa zinajumuisha, utoaji mafunzo katika elimu "kwa mtazamo wa kuasisi watu wenye kukashifu kwa ajili ya kupanda thaqafa ya kidemokrasia" ndani ya mujtama.

Ajenda hii ya kuwafanya vijana Waislamu kuwa masekula pia yaweza kuonekana waziwazi katika sera na matendo yanayo fanywa na serikali za kisekula. Nchini Uingereza kwa mfano, Julai iliyopita, serikali ilileta Mswada wa Kupambana na Ugaidi na Usalama (CTS) uliolifanya jukumu la kisheria juu ya walimu, madaktari, wafanyikazi wa kijamii, serikali za mitaa na hata chekechea kufuatilia dalili zozote zile zinazoitwa "zisizokuwa za misimamo mikali" kwa watoto Waislamu na endapo kuna udharura kuwapeleka katika 'kituo' cha serikali cha mradi wa kupambana na misimamo mikali. Wale wazazi Waislamu watakao shukiwa kukuza fikra za Kiislamu zinazoitwa za misimamo mikali watakabiliwa na hatari ya kupokonywa watoto wao na kuwekwa chini ya uangalizi wa dola. Mswada huo wa CTS, ambao ndio kilele cha mkakati wa muda mrefu wa serikali ya Uingereza wa KUKINGA dhidi ya misimamo mikali, kimsingi umewalazimisha wale wote wanaofanya kazi na watoto wa Waislamu kuwatazama kama wenye uwezo wa kuwa magaidi na kupitia muangalio wa uhalifu. Ni mkakati ambao umechafua imani na amali msingi za Kiislamu kwa watoto wa Waislamu na jamii nzima kwa jumla kwa fimbo ya 'misimamo mikali'. Kwa mujibu wa tarakimu rasmi zilizo chapishwa na Baraza Kuu la Kitaifa la Polisi, tangu 2012, nusu ya watu 4000 ambao wamepelekwa katika Kituo cha mradi huo wamekuwa chini ya umri wa miaka 18. Watoto 1500 kati ya umri wa miaka 11 na 15, na 400 chini ya miaka 10 pia wamepelekwa, huku mdogo wao zaidi akiwa na miaka 3 tu. Sababu za kushukiwa zinajumuisha kuomba kuswali au kufunga wakiwa shuleni, kutotaka kuhudhuria masomo ya muziki au kuchanganyika na jinsia ya pili, kuvaa beji ya 'Iacheni Huru Palestina', wasichana kuanza kuvaa vazi la Kiislamu la hijabu, au hata watoto kusema Alhamdulillah! Mvulana mmoja wa shule alihojiwa na polisi baada ya kuingia na toleo linalo pigia debe kususia umbile la Kiyahudi shuleni, huku mwengine aliye zungumzia kuhusu hadhara ya Kiislamu iliyopita katika mradi wa utafiti wa kimasomo wa shule alisemekana kuwa na maoni ya misimamo mikali. Vyuo Vikuu pia vimeagizwa kung'oa fikra za 'misimamo mikali' kutoka katika vitivo vyake. Serikali yenyewe imeweka wazi kile inacho kiita kuvuka mipaka au misimamo mikali – ikiwemo kupinga sera ya kigeni ya Kimagharibi katika ulimwengu wa Waislamu; kukataa demokrasia ya Kimagharibi, maadili huru, ubaradhuli au usawa wa kijinsia; utekelezaji sheria za Kiislamu za kijamii kama vile kuwatenga wanaume na wanawake au kuvaa niqab, na kuunga mkono fahamu ya Ummah wa kiulimwengu, Shari'ah au Khilafah.

Dola nyinginezo za kisekula pia zimeonyesha ufuatiliziaji huu mkali na kulenga imani za Kiislamu za vijana Waislamu – kupitia kutiwa usekula mitaala ya elimu; kuwafanya wahalifu wale vijana wanao lingania Uislamu; na kuingilia usomeshaji wa Uislamu katika madrassa chini ya kisingizo cha urongo kuwa ndio 'mazingira murua ya ugaidi'. Nchini Pakistan Januari hii, vyombo vya habari vilitangaza kuwa serikali ya Punjab imepiga marufuku kulingania Uislamu katika vitivo vya vyuo vikuu. Hatua hii ni sehemu ya Mpango wa Kitaifa wa Utendakazi wa serikali hiyo ambayo imezuia udhihirishaji wa Uislamu katika vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na majukwaa ya kisiasa ikituhumu kuwa ni "matamshi ya chuki" au "misimamo mikali". Vilevile imezifunga zaidi ya shule za Kiislamu 180 nchini humo, na kuufanya ulinganizi wa kutabikisha Uislamu kuwa ni uhalifu ikipelekea kukamatwa kwa maelfu ya Wanazuoni, wanafunzi, wahitimu, walimu na Waislamu wengine wenye ikhlasi katika dola hiyo. Bangladesh pia imefuata njia kama hiyo, kukamata, kuteka nyara, na hata kutesa wanafunzi na wahitimu wasiokuwa na idadi wanao lingania Uislamu nchini humo, ikiwemo dada wawili wadogo Waislamu ambao waliteswa kinyama kwa kugawanya matoleo yanayo alikia kongamano la mtandaoni kuhusu jinsi Uislamu ungeweza kutatua matatizo ya kisiasa na kiuchumi ya nchi hiyo. Mnamo Januari mwaka huu, Chuo Kikuu cha Dhaka kiliwafukuza wanafunzi 7, kwa kuwa tu wabebaji ulinganizi (da'wah) wa Uislamu. Zaidi ya haya, serikali sugu ya kisekula ya Hasina imeilazimisha Bodi ya Kitaifa ya Elimu kuondoa nususi zinazo husiana na Uislamu na kuzibadilisha kwa maandiko kuhusu ibada na imani za Kihindu. Kati ya nususi 193 hizo ambazo zinafunzwa kuanzia darasa la 1 hadi 10, 137 yake zina maalumati kuhusiana na upagani na kazi zinazo husiana na mwelekeo wa kutoamini Mungu. Na nchini Tajikistan dada zangu, bunge hata lina jadili kupiga marufuku majina ya Kiislamu kwa watoto ili kupambana na ongezeko la kushikamana kwa idadi ya raia wake Waislamu na watoto wao na Dini yao. La hawla wala quwata illah Billah!

Pamoja na yote haya, dada zangu, dola zisizo kuwa za Kiislamu katika ulimwengu wa Waislamu zina pigia debe kwa nguvu vyombo huru vya habari vya Kimagharibi nchini humo ambavyo vinaeneza fikra chafu mno na miondoko miovu ya kimaisha kwa vijana wa Kiislamu, na kufanya kazi kwa bidii ili kuwapagawisha kwa mtindo wa usanii wa burudani, pamoja na kushambulia fikra za Uislamu na kuzihusisha na ghasia au ukatili. Nchini Indonesia kwa mfano, kumekuweko na ajenda kali ya vyombo vya habari iliyo tekelezwa na vyombo huru vya habari kwa mwaka wote huu uliopita ili kupigia debe fikra huru kama vile ubaradhuli kwa vijana, pamoja na kutia

*Endelea Uk..4*

hofu juu ya Shari’ah ya Kiislamu.

Dada zangu wapendwa, kutokana na yote haya, ni wazi kabisa kuwa kuna ajenda kali ya kuwafanya vijana wetu kukumbatia kitambulisho huru cha kisekula na kuwa mabalozi wa mfumo na nidhamu ya Kimagharibi. Ni kuwafanya kukataa fikra msingi za Kiislamu za kijamii na kisiasa na kuachana na amali msingi za Kiislamu kupitia kuwanasibisha na ‘misimamo mikali’ au ‘itikadi kali’ na kuunda kizazi cha Waislamu cha usoni kilicho hofishwa kwa kukaa kimya, na kuwa na uoga mwingi wa kuzungumza kwa ajili ya Ummah wao au Dini yao. Na ni kuwafanya wakubali sura iliyo geuzwa ya kisekula ya Uislamu ‘poa’ na kuiona Imani yao kuwa si chochote isipokuwa isiyofaa, iliyo pitwa na wakati, dini katili ambayo haipaswi kuhusishwa na chochote katika maisha ya ulimwengu wa kisasa.

Lakini dada zangu, kama Ummah, pia twahitaji kuchukua jukumu kwa ajili ya mgogoro huu wa Utambulisho unao athiri vijana wetu. Kwani tulipokuwa na ulegevu katika kufahamu na kutekeleza Uislamu maishani mwetu na kuachana na utabikishaji wa hukmu na nidhamu yake, Khilafah, katika biladi zetu, ndipo ikaruhusu fikra zisizokuwa za Kiislamu – za jadi na za kisasa – kuingia katika majumba, jamii na mujtama zetu. Fahamu za kuhisabiwa na Mwenyezi Mungu (swt), hayah katika mavazi na vitendo, kujitolea kwa Akhera juu ya Dunia, mpangilio maalumu wa akhlaq maishani ulio fafanuliwa na Muumba, na ufahamu safi wa suluhisho la Uislamu kwa matatizo yote ya maisha na ulimwengu huu – zikachujuka na kudhoofika katika jamii na biladi zetu. Hili lilipelekea watoto wetu kuvutiwa na kuitazama thaqafa na nidhamu huru inayo tawala inayo wazunguka, kutafuta majibu kwa ajili ya matatizo yao na jinsi ya kuendesha maisha yao. Wengi pia walikuja kuutazama Uislamu kama tu mkusanyiko wa ibada na hukmu na hivyo kutofaa maishani mwao, huku wengine wakichukia au kuwa na shaka na Imani zao za Kiislamu, ikipelekea kuachana na Dini yao. Hivyo basi, watoto wetu walikuja kuathirika na maovu na matatizo yale yale kama ya Magharibi. Nchini Uturuki kwa mfano, kati ya watu 22,000 waliopokea matibabu kutokana na ulevi na utumizi wa mihadarati mnamo 2013, takriban asilimia 60 walikuwa na umri kati ya 15-17, huku robo wakiwa na umri kati ya 12-14. Wengi wa vijana wetu pia walijitenga na matatizo ya jamii yao na Ummah na kujitenga na jukumu lao la kuleta suluhisho kwa kadhia hizi kupitia Dini yao.

Dada zangu wapendwa, kutatua mgogoro huu wa utambulisho katika vijana wetu na kufahamu jinsi ya kuwatayarisha ili kukabiliana na changamoto nyingi wanazo kumbana nazo katika kushikamana na Dini yao na kuchukua dori yao halisi kama walezi na walinzi wa Uislamu ni moja ya mambo muhimu zaidi kwetu sisi kama Ummah leo. Ni lazima ichukuliwe kama mada ya kipaumbele katika ajenda yetu na jambo ambalo ni lazima tutie juhudi zetu zote ili kufahamu na kutatua kwa uwazi na haraka ili tusikipoteze kizazi cha usoni cha Dini yetu pamoja na Akhera yetu na ya watoto wetu. Mwenyezi Mungu (swt) asema,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

“Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na jamaa zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe” [Al-Tahrim: 6]

**Imeandikwa na**

**Imrana Mohammed**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya**
**Habari ya Hizb ut Tahrir**

**na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika**
**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Kuwafanya Vijana Waislamu kuwa Masekula kupitia Mitaala ya Elimu

**Hotuba ya Pili Katika Kongamano: 'Vijana Waislamu …Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi'**

Thaqafa ya watu wowote huwakilisha uti wa mgongo wa uwepo wao na kudumu kwao. Juu ya thaqafa, hadhara yake hujengwa, dhamira na malengo yake hufafanuliwa, mpangilio wa maisha yao huwa wa kipekee kwake, watu wake huyeyushwa ndani ya chungu kimoja ili watafautishwe kupitia hiyo na mataifa na watu wengine. Njia ya kuhifadhi thaqafa ya Ummah ni elimu inayofanya kazi kujenga aqliya na nafsiya, na kukuza maadili, fikra na misingi ambayo kwayo utambulisho wa mtu huundwa katika mustakbali. Na kwa kuwa uhusiano kati ya udhibiti na elimu ndio msingi wa Magharibi, wamefanya kazi kuzidhibiti biladi za Kiislamu na kuzitawala kupitia kuifanya elimu kuwa ya kisekula, kama walivyo fanya kazi kuwaweka mbali Waislamu kutoka katika Dini ya Uislamu ili kuzuia uzalishaji wa utambulisho wa Kiislamu uliobeba hamu kwa Ummah na kadhia yake nyeti. Kwa sababu hii, wamejitokeza kukarabati mitaala ya elimu kwa mujibu wa mtazamo wao wa utandawazi na mielekeo ya kisekula. Hivyo, mitaala ya elimu sio tena jambo la kindani katika biladi hizi bali limekuwa ni jambo la kiulimwengu lenye lengo la kumomonyoa Itikadi (Aqeedah) ya watu wake na kuwasafisha mabongo yao kutokana na fikra na maadili. Na hilo limefanya mitaala hii ijengwe juu ya msingi mwengine usiokuwa Aqeedah ya Ummah. Bali imejengwa juu ya Itikadi (Aqeedah) ambayo inagongana nayo, ambayo kwayo inataka kugurisha thaqafa ya Kimagharibi kwa vijana na mabinti wa Ummah huu, tofauti na thaqafa ya Ummah wao ambapo ni njia hii ndio inayo dhamini utiifu kwao … Kasisi Dkt. Samuel Zwemer, akielekeza hotuba yake kwa wamishenari, alisema, "Mumewatayarisha vijana katika biladi za Waislamu ambao hawajui tena fungamano na Mwenyezi Mungu na hawangependa kulijua. Mumewatoa Waislamu kutoka katika Uislamu huku mukiwa hamkumsababisha kuingia kwao katika Ukristo. Zaidi ya hayo, yule aliyelelewa katika Uislamu amejitokeza kwa mujibu wa vile ukoloni ulivyotaka awe; hajali juu ya majanga na anapenda starehe na uvivu huku hamu yake maishani ikiwa haifuati isipokuwa matamanio yake".

Katika mchakato huu wa kuingiza usekula wametumia njia kadhaa ikiwemo kuangazia juu ya kupuuza lugha ya Kiarabu, na kuwaweka wanafunzi mbali nayo, huku wakiufanya ufundishaji wa lugha za kigeni sawa au hata juu kuliko Kiarabu. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya kuwaondoa ufahamu wa Ahkam za Qur'an (katiba yao) kwa njia ambayo ingeangazia kufikiria kwao na kuwafanya kutia bidii kwa ajili ya mwamko. Walifanya vivyo hivyo katika masomo ya Kiislamu kupitia kuyafanya kuwa ni masomo ya upili badala ya kuwa ni masomo ya msingi. Na huku ufundishaji wake ukiwa katika muundo wa kazi ya ziada ya nyumbani, kaida na kuwa somo linalo hitajika tu kupita mitihani kabla ya hatimaye kusahauliwa, badala ya kuwa liwe ndio msingi wa kujenga utambulisho wa Kiislamu kwa vijana. Na usisahau mtego wa elimu ya Kimagharibi na shule za kigeni, ambapo wamishenari wa Kikristo au wa kisekula, ambao kihakika ni kama vyombo vya kutia sumu yao hatari katika Dini, fikra, fahamu na tabia … Hivyo basi, matunda ya yote haya, yalikuwa ni kujenga msingi juu ya fikra huru, ambazo zilikuwa si za Kiislamu. Yote haya, huku Uislamu ukitazamwa kana kwamba ni dini ya kikasisi tu iliyotenganishwa na maisha na ambayo ilihusishwa na ibada pekee na sio katiba na njia ya maisha, kuongezea na kutokuwa na uhusiano au umuhimu kwake na maisha yao ambayo ina athari juu ya fahamu na tabia zao … Mwanamke alikuwa na mgao wake kuhusiana na mabadiliko haya ndani ya mtaala huo; walifanya bidii kubadilisha sura na dori yake msingi ndani ya mujtama, ambayo waliita 'Kubadilisha Unyanyapaa Wake!' kupitia kumfanya ang'ang'ane kuwa mwanamke mchapakazi pekee na sio mke nyumbani. Hivyo basi wakalitoa somo la usimamizi nyumbani nje ya mtaala huo, ambalo linajumuisha ndani yake mada ambazo zingemsaidia msichana kupata elimu kuhusu dori yake msingi. Pia wakatangaza vita dhidi ya kile wanachokiita 'ndoa ya mapema' huku wakiimba kuhusu umakinifu wake wa kiuchumi na uhuru wake. Wakawashajiisha wanafunzi kujihusisha katika amali, safari, miradi na vyama ndani na nje ya shule kama vile matukio na sherehe zisokuwa za Kiislamu, ambazo aghalabu huhusisha kuchanganyika baina ya wanaume na wanawake, zikionyesha miili na ukiukaji wa hukmu za sheria.

Ndio, dada zangu … Wanataka kudhamini kukuuza kizazi ambacho kwa jina ni cha Waislamu lakini kidhati na kimsingi ni cha kimagharibi. Kizazi ambacho kitaishi katika biladi ya Kiislamu lakini kitamiliki ada na maadili ya mujtama wa kimagharibi. Kizazi ambacho ni watoto wa 'Umar, Ali na Salahuddin lakini chenye kuamini kuwa kila ulinganizi wa kurudisha Uislamu halisi una wakilisha ulinganizi wa ugaidi, urudishaji nyuma, na upotofu, na wala sio ulinganizi wa mwamko. Na ili wasimame wenyewe kuwa kizingiti mbele ya kurudi kwa Uislamu na dhati yake.

**Dada zangu waheshimiwa:**

Wakoloni wamezikadiria sera za elimu kuwakilisha moja ya sehemu muhimu ambazo ni lazima wazidhibiti juu yazo. Hivyo wanaingilia mitaala, shule na sera za elimu katika biladi kadhaa kama Misri, Pakistan, Saudi Arabia na Yemen. Kwa mfano, usaidizi mkubwa ambao Amerika imetoa kwa serikali ya Musharraf nchini Pakistan ili kuzifuatilia madrassa na kuvipiga marufuku vitabu vya

*Endelea Uk..6*

shule katika masomo yote kutokana na uhusiano wake wowote na Uislamu. Hii ikiwemo kufuta mada ya Al-Walaa' Wa-l-Baraa', Ayah za Jihad na kuchafua baadhi ya ufafanuzi wa Itikadi (Aqeedah) ndani ya sayansi ya Shari'ah nchini Saudi Arabia. Yote hayo, kwa mujibu wa madai yao na visingizio vyao, yanafanywa ili kuzuia 'ugaidi' kuibuka katika madrassa hizo!! Vile vile, nchini Palestina na baada ya kuwasili kwa yale yanayoitwa 'Mamlaka ya Palestina' mitaala imebuniwa inayofanya kazi kuuvunja Uislamu ndani ya nafsi za vijana Waislamu na kuwabadilisha kuelekea ukafiri wa usekula kupitia kuzivuruga akili zao kwa fahamu zilizo mbali na Uislamu. Ama kwa Misri Al-Kinanah, wamefuta nususi zote zinazo husiana na vita kwa Mayahudi huku zikitukuza amani na maelewano. Pia wamefuta masomo yanayo jadili watu wenye utambulisho wa Kiislamu kama Salah ud-Deen Al-Ayubi na 'Uqbah Bin Naafi' wakidai kuwa masomo haya yanachochea misimamo mikali na ghasia huku wakifuta zaidi Hadith za Mtume (saw) zinazo shajiisha Jihad. Hii ni ikiongezewa na kurudia hadhara ya Kifirauni kama mwakilishi wa historia ya Misri huku wakipuuzia kwa ukamilifu ufunguzi wa Uislamu katika historia yake yote.

Ama kwa hapa Tunisia, Bourguiba alikipiga marufuku Chuo Kikuu cha Zaytuna na kubuni shule ambazo mwelekeo wa kisekula wa kimagharibi umetawala. Aliingiza ufundishaji wa lugha za kigeni katika umri mdogo, huku akiwaweka mbali wanafunzi kutoka na elimu ya Kiislamu akiibadilisha kwa thaqafa ya kijamii ambayo kwayo mwanafunzi atafunzwa sheria za kibinadamu na mafungamano fisidifu kama uzalendo na utaifa.

Kamwe hatutadharau dori ya mashirika ya vijana, vyama vya wanawake na taasisi za kimagharibi kama USAID, UNICEF, UNESCO na Baraza la Uingereza, ambayo upande mmoja yanatoa usaidizi kwa wanafunzi na elimu na ustawi, huku kindani (na kwa uhalisia) yakiwa na sumu hatari kupitia kutia usekula fikra na fahamu. Hii ni kiasi kuwa mazingira na anga jumla ndani ya shule hizo yawe ya kikafiri na haswa yawe ya kisekula, ambapo Magharibi inapewa sura nzuri na ya kuvutia huku Uislamu ukionyeshwa kuwakilisha mafungamano na mipaka inayozuia uhuru, kuregesha nyuma na ni kikwazo kwa maendeleo na mwamko. Sura inayotolewa ni Magharibi inawakilisha maendeleo, ufanisi na hadhara tajiri ambayo inapaswa kufanya bidii kuwa kama wao na kuendelea mbele kupitia njia yake!! Hivyo tunawaambia kuwa Mwenyezi Mungu Ta'ala amesema:

وَلاَ تَرْكَنُواْ إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُواْ فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللّهِ مِنْ أَوْلِيَاء ثُمَّ لاَ تُنصَرُونَ

"Wala msiwategemee wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa" [Hud: 113].

**Dada zangu waheshimiwa:**

Hii ndio hali ya sasa ya elimu ndani ya biladi za Waislamu na hivyo tufanye nini kuhusiana na vijana na wanafunzi wetu?! Ni ipi njia sahihi ili tuwafunze watoto na wanafunzi wetu Uislamu ima kama wazazi au walimu?

Kama tulivyo taja, hatupaswi kuingiliana na Uislamu wa sasa juu ya msingi kuwa ni somo tu la kusomwa au kupata maalumati yanayo jaza karatasi za mtihani na mwanafunzi kupata shahada kupitia kwayo, huku ikiishia hapo. Bali, ni lazima tukuze fahamu zinazo pelekea mabadiliko ya kifikra na baada ya hapo mabadiliko ya tabia na mwenendo. Ni lazima tuwaunganishe na uhalisia ili uwaguse na kuufahamu ili kuharakisha utekelezaji wake … Hivyo tunapowapa somo lolote kama 'Ibaadat (vitendo vya kiibada) au Akhlaq (maadili), ushairi, historia au sayansi, sio mujarrab tu wa kupeanwa kama elimu ya nadharia pekee. Bali tutaiunganisha na uhalisia na Ahkam Ash-Shari'ah ambazo zitawanufaisha katika kujenga fahamu na tabia au mwenendo wao.

Hivyo kwa mfano, tunapo ifafanua Swala, hatuwafunzi tu ni Rakaa ngapi, tunasema na kufanya nini, bali kuwa ni nguzo (Rukn) ya Dini na kuwa kupitia kutengea kwake kitendo hutengea na kwamba ni lazima iwe yenye kukataza na kukinga kitendo chochote kiovu na kichafu. Na tunapo wafunza usomaji wa Qur'an, tunapanda ndani yao kuwa inawakilisha katiba (Dustoor) ya maisha ya kujifunga na kuitekeleza, na kwamba sio tu ya kusomwa wakati wa Ramadhan, mazishini au kabla mitihani. Kwa kuwa inawakilisha Ahkaam Shariah zinazotakiwa kujifunga kwazo na kuzitekeleza katika ngazi ya mtu binafsi na dola… Hivyo hivyo pia kuhusiana na mambo ya kimaumbile yanayo somwa katika sayansi ambapo kwa mfano hatutayaunganisha tu kwa matendo ya kimada pekee bali pia tutawasilisha upande wa Kiimaani kwa kuyaunganisha na Muumba wake (swt) kama yalivyo jitokeza katika Ayah za Kitabu chake Kitukufu. Hivyo hivyo pia kwa Akhlaq, Muamalaat, historia, fizikia na teknolojia miongoni mwa masomo mengine kupitia kuyaunganisha kwa njia ya kuendelea na thaqafa ya Kiislamu, Aqeedah na Ahkam, na fahamu na tabia…

Najua dada zangu kuwa jambo hili si rahisi kiuhalisia kwamba tunakabiliwa na vita dhidi ya Uislamu na waumini wake. Lakini, ni wajib juu yetu kupunguza madhara yanayo tokana na vita hivi. Najua kuwa utekelezaji wa Uislamu unakosekana kutokana na kukosekana dola ya Kiislamu inayo utabikisha kwa upana na ukamilifu… Ni dola hii ndiyo itakayo dhibiti ndani yake elimu ambayo mtu anaihitaji katika uwanja wa vita vya kimaisha kama wajib. Ni jukumu lake kutoa elimu bila ya malipo kwa kila mtu, mume au mke, katika viwango vya msingi na upili. Hii ni huku ikifungua fursa kwa elimu ya zaidi na ya juu bila malipo kwa wote kwa kadri ya uwezo wake… Sio kama hali ilivyo sasa ambapo watu wakati mwengine hujinyima chakula chao ili waweze kuwapa watoto wao elimu!! Ni dola ambapo lengo la elimu liko juu ya mambo mawili:

La kwanza ni kujenga utambulisho wa Kiislamu, aqliya

*Endelea Uk..7*

na nafsiya, na hilo ni kupitia kukuza thaqafa ya Kiislamu kama Aqeedah, fikra na tabia ndani ya akili za wanafunzi na nafsiya zao za ndani. Kwa sababu hiyo, wale wanao andaa mitaala na kuitekeleza ndani ya dola ya Khilafah watakuwa makini kufikia lengo hilo…

Jambo la pili ni utayarishaji wa watoto wa Kiislamu ili watoke miongoni mwao wasomi wanao chukua taaluma katika kila nyanja ya maisha ima iwe katika sayansi za Kiislamu (kama Ijtihad, Fiqh na Mahakama miongoni mwa nyanja nyenginezo) au katika sayansi za kiutafiti (kama uhandisi, kemia, fizikia, utabibu na nyenginezo), wasomi wenye uwezo watakao ibeba dola ya Kiislamu na Ummah wa Kiislamu mabegani mwao ili ichukue nafasi ya kwanza ya uongozi miongoni mwa mataifa na dola za ulimwengu. Hapo ndipo itakapo kuwa dola inayo ongoza, dola iliyo barabara na mfumo wake, na sio dola ya kitumwa na kibaraka katika fikra na uchumi wake kama hali ilivyo sasa katika ulimwengu wa Kiislamu na Kiarabu… Itakuwa ni Dola ambapo shule itakuwa ndio chimbuko la kwanza la ujenzi wa watu wenye utambulisho wa kipekee wa Kiislamu, katika nyanja za Usool ul-Fiqh, lugha na Tafseer. Kama itakavyo kuwa chimbuko la kwanza la ujenzi wa watu waliomakinika katika nyanja za elimu inayohusiana na chembe (atom), anga na tarakilishi nk…. Ni dola ambayo sote tuna hamu ya kuishi ndani ya boma lake na chini ya kivuli chake…

Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kuharakisha kurudi kwa Khilafah kwa njia ya Utume ili watoto wetu waweze kusoma chini ya kivuli chake na kuondolewa fikra za kirasimali pamoja na ufisadi na madhara yake yote… na twataraji kuwa siku itakuwa karibu…

**Muslimah (Umm Suhaib) Ash-Shaami**

# Vijana Wanawakilisha Fursa Nzuri Zaidi

**Hotuba ya Tatu Katika Kongamano: 'Vijana Waislamu…Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi'**

Dola, mashirika na mujtama za kibinadamu kwa muda mrefu zimekuwa zikishughulishwa na vijana – hili ni kweli leo na litaendelea kuwa kweli. Hii ni kutokana na yale yaliyomo katika rika hili kuhusiana na maendeleo ya kimwili na kiakili, yanayo ufanya umri huu kuwa tayari zaidi na kudhihirisha uchangamfu, nguvu, ubunifu, mafanikio, uongozi, ari, uvumilivu, ukarimu, kujitolea na maendeleo miongoni mwa sifa nyenginezo nzuri.

Katika thaqafa ya utandawazi tunayoishi ndani yake leo, inadhihirika kuwa neno 'vijana' linahusishwa katika akili za wengi na rika ambalo kiwango kikubwa cha anasa za kimwili hutafutwa, na mapenzi ya kupenda starehe, mzaha na kukesha (au kupoteza wakati) ndio mambo makuu ndani yake. Hili humulikwa na hamu ya ladha tofauti tofauti za michezo na sanaa. Ni rika hili la maisha ambalo kampeni ya mauzo ya Kampuni ya Coca Cola imelikusanya katika mwito wao wa mwaka huu. "Furahia Wakati". Kampuni hii kubwa haikuandaa tu mwito huu pekee bali pia uliandamana na mbinu ya kimakusudi ya kuandika neno 'Coca-Cola', kwa muundo maalumu wa mduara mwekundu, muonekano wa kinje wa chupa hiyo na kikosi cha wasanii waliochukuliwa kupigia debe bidhaa hii. Kampeni ya vyombo vya habari ya kiulimwengu hufupisha ujumbe wake kwa kubeba maadili yake pamoja na filosofia ya kimagharibi kuhusu maisha kuhusiana na fungamano la mwanadamu na ulimwengu na maisha kwa sekunde kadhaa.

Vyombo vya habari vimemnyamazisha yule aliye matatani ili asalimu amri kwa ujumbe wake, aufuate na akubali yaliyomo katika jumbe zozote fiche. Mujtama katika biladi za Waislamu zimekuwa mujtama dhaifu za watumizi baada ya kuwa za uzalishaji na maendeleo. Tatizo haliko katika utamaduni wa matumizi pekee bali linapanuka hadi kwa ufisadi wa dola na mmomonyoko wa utambulisho. Vyombo vya habari vya runinga za Kiarabu, tangu mwanzoni mwake, vimemuonyesha kijana mdogo, akipambika na thaqafa ya kimagharibi katika mazungumzo, mavazi na mitizamo yake, kama mwakilishi wa maendeleo, aliye imara na mwenye furaha. Na huku yule aliye jifunga na Uislamu akionyeshwa kama mtu aliye na utambulisho usioimara na dhiki. Inawakilisha uvundo wa vyombo vya habari ambavyo havina utambuzi wa tofauti baina ya thaqafa ya kijana wa Kiislamu anaye tafakari, kuingiliana, kuzalisha na kufanya kazi ndani ya mpangilio wa Hukm Ash-Shar'i ili kuangaza njia yake, na baina ya "Furahia Wakati" ambayo ina ishi kwa muda huu tu huku ikifunga furaha kwa hisia za muda mfupi tu au kwa starehe au shibe ya mwili tu. Lakini ni upenyaji wa kithaqafa na utandawazi wa kifikra unao lazimishwa kwa nguvu juu yetu katika ulimwengu wa Kiislamu, unao tafuta kuzifanya fahamu zao kuhusu maisha zinazo chipuza kwengineko kando na mfumo wetu, Dini tukufu ya Uislamu, fahamu ambazo tunazi tabanni, kuzihami na kufanya kazi kuzimakinisha ndani ya mujtama zetu, hata kama zina kinzana na Aqeedah yetu na mtazamo wetu kuhusu maisha.

Vyombo vya habari hutoa taswira ya vijana kama rika lenye kupatiliza wasaa wa furaha na kujitolea nafsi zao kutafuta starehe huku wakati huo huo vikienda hadi kileleni kuhusu uhalisia wa masaibu ya vijana na matatizo yao kuhusiana na ukosefu wa ajira, muda wa faragha, upotezaji wakati, na shinikizo la mawazo. Vinawazingira vijana kwa sura mbovu, za uhalifu, mihadarati, muozo na akhlaqi fisidifu na kuziangazia tabia hizi na miondoko hii miovu hadi hili likageuka kuwa fikra ya kudumu inayo pachikwa juu ya vijana na kuongezea katika masaibu yao. vyombo hivi vya habari havijaribu kupanda sura nzuri inayo eneza matumaini na kuwaonyesha vijana kuwa umri huu maishani huwakilisha umri wa mafanikio, ufanisi na maendeleo. Na hilo ni kwa sababu vyombo hivi vya habari havifanyi kazi kuunyanyua Ummah huu.

**Dada zangu waheshimiwa…**

Leo ulimwenguni kwa kuwepo na maendeleo endelevu ya mbinu za uunganishaji na mawasiliano, uwezo wa mtu anaye miliki pesa na ushawishi wa kueneza fikra zake na kuzipigia debe umekuwa ni mkubwa. Runinga, redio na vyombo vya uandishi wa habari kwa aina zake tofauti tofauti vinapenya ulimwengu kuanzia sehemu yake ya mbali hadi sehemu yake ya karibu bila ya vizingiti vyovyote vikuu. Na hivyo vinaingia kila nyumba, sauti yake inasikika na kila sikio huku picha zake zikinasa kila jicho. Miundo hii ya vyombo vya habari inafanya kazi ya kutuma ujumbe kwa vijana katika hatua ya kuvuruga fikra. Hivyo haviwasilishi matatizo halisi ya maisha ya kila siku kwa njia ya umakinifu, huru na isiyo ya mapendeleo na endapo vitafanya hivyo basi itakuwa tu kwa lengo la kuchukua mwelekeo ule ambao mmiliki wa kituo au chombo cha habari, chochote kile, anaridhika nao. Vinafanya kazi katika kuamsha hisia (ghariza) na kuchochea hamasa na kuziamsha pasi na haja au manufaa yoyote yanayo tarajiwa, vikiwa havitoi chochote ila ushawishi muovu. Uharibu wa kimpango kupitia mechi za mpira za nchini, barani na kimataifa unaendelea takriban kwa njia ya kudumu. Mechi moja au shindano moja halimaliziki isipokuwa hufuatwa na jengine. Yeyote anaye okoka kutokana na mapenzi ya mpira huwasilishiwa miereka, mashindano ya magari na aina nyengizezo tofauti tofauti za upotezaji wakati. Hatusikii kutajwa kokote kwa ndugu zetu wa Cameroon, Ivory Coast au Gambia isipokuwa tu ndani ya muktadha

*Endelea Uk..9*

wa Kombe la Afrika, kana kwamba mafungamano ya udugu yamefungika na misururu ya mpira!!
Yule ambaye havutiwi na michezo huambiwa ni lazima atawale ulimwengu kwa talanta zake za kindani katika uimbaji, uchoraji, uchezaji densi, maonyesho ya fesheni au uigizaji. Katika yote haya, yuko tayari kutumia pesa zake na wakati wake sambamba na watumizi wengine. Humhadaa na kumtongoza kutafuta talanta katika kujiachia na kufanya upuzi ili apoteze muda wake katika utafutaji wa kila kitu ambacho si chema. Vipindi vya runinga, mashindano na amali za kutafuta talanta za kisanii zimeshindwa kutatua misongo ya mawazo kwa wenye talanta za kikweli na wale wanaofanya kazi katika nyanja za utafiti wa kisayansi na uvumbuzi, na wale wanao fuzu. Vyombo vya habari huwapumbaza vijana huku uhamisho wa maarifa ukiendelea na maandamano ya wanasayansi na wale wale walio werevu wakiendelea kuondoka katika ardhi zilizo kataa kutambua kufaulu kwao na kuwavunja moyo kuhusiana na talanta zao.

Vyombo vya habari vimechafua sura ya mujtama ndani ya ardhi za Waislamu, kuharibu uhalisia wa kikweli na kufisidi mitizamo ya vijana huku vikimulika sura inayo gongana na uhalisia wa mujtamaa huu. Hivyo mwanamke akawa na ubinafsi na kuharibika na hana hamu nyengine isipokuwa kujipodoa uso wake, fesheni na vipindi vya upishi, huku mwanamume akiwa mbinafsi na kuzongwa na mahusiano mengi, huku mahusiano ya kijamii yakijengwa juu ya mada, manufaa na mitazamo ya kimakosa na hamasa za kirongo. Kufikia hapa naweza kukumbuka Kitabu cha Nyimbo cha Abu al-Faraj al-Isfahani, kitabu kilicho kusanya mashairi na maongezi yaliyo chafua historia ya zama za mwanzo za Uislamu na sura ya Zama za Dhahabu za hadhara ya Kiislamu iliyo yajaza macho na masikio na kuushangaza ulimwengu kwa jumla, alipoifunga kwa wafanyi kazi, makasri na mapungufu ya wafalme! Mujtama wa Waislamu ulionyeshwa kuwakilisha mujtama lemavu ambao pumbao na matamanio yalitawala ndani yake. Mujtama ulioishi kwa wasaa uliopo tu na 'Kufurahia Wakati'. Hatupaswi kupuuza kuwa toleo la kwanza la kitabu hiki lilichapishwa Magharibi; watu wenye kasumba ya umamboleo walikuwa na hamu nacho na kusajili jeshi la wanaochunguza na wanaokashifu ili kunyanyua hadhi yake kwa malengo yao wenyewe.

Leo ulimwenguni, dola hucheza dori kubwa na msingi katika kuvisaidia vyombo vya habari katika kutekeleza dori yake. Hivyo basi, ni dola ndio inayotoa leseni kwa vyombo vya habari vya kibinafsi kutekeleza kazi yake na kuvisaidia kimaadili. Hii ni katika hali ambapo serikali sio mmliki halisi wa vyombo vya habari na msingi wa usaidizi wake. Kile ambacho vijana wetu wanafikishiwa katika nchi zetu za Kiislamu, kwa maana nyengine, ni mpangilio wa shambulizi lililo andaliwa linalotafuta kumakinisha fahamu ambazo zinagongana na mtazamo wetu kuhusu maisha. Wanawafanya vijana wetu, watoto wetu wenyewe, kutothamini juhudi zetu za haraka. Hizi ndizo juhudi zilizo anza kuleta matunda katika mchakato mkubwa wa mabadiliko na mapinduzi yenye baraka ya Ummah ambayo cheche yake ilianzia nchini Tunisia 'kheri ya kijani'. Dola za kikoloni na walinzi wa utandawazi wamesimama nyuma ya mpangilio huu wa kififkra na kuusaidia kiakhlaqi na kimada. Wamiliki wa vituo vya runinga vya kibinafsi na vyombo vyenginevyo vya habari, ambao wametabanni fikra yao na kutembea barabara yao, wanawakilisha uongozi kuhusiana na utekelezaji wa shambulizi hili. Wanaosimama pamoja nao na kihakika mbele yao ni tabaka la viongozi katika nchi za Waislamu ambao wametabanni njia na fikra hizo hizo, kuwawezesha kueneza ufisadi wao na thaqafa mbovu tunayo ishuhudia leo.

Ujumbe wa vyombo vya habari unao kaririwa ni 'Nyinyi tuachieni sisi na msiondoke kutoka katika kochi mwanana la mahmeli … Kwa nini mukimbilie kutenda ilhali mwaweza kuona, kujadili, kupika, kucheza michezo yote huku mukiwa mbele ya runinga? Kwa nini mukimbilie kutenda ilhali iko ndani ya uwezo wenu kutekeleza uhamasishaji wa kisiasa na kuingiliana na matukio, wakati ambapo mwaweza kukaa juu ya kochi lenu la mahmeli mukitazama runinga na kutumia mitandao ya mawasiliano?' Ni kana kwamba vyombo vya habari vinawataka vijana kuachana na dori zao kama waanzilishi wa mageuzi ya kikweli na badala yake kukubali starehe bandia, kupoteza umri mzuri zaidi wa maisha yao na kutokubali jukumu lolote. Kana kwamba vijana hawaaminiwi na kustahiki kutekeleza hilo.

**Dada zangu waheshimiwa…**

Mtoto anapo lelewa katika kuzikumbatia simu za kisasa na michezo pasina nidhamu au udhibiti na kuwa kijana pasina mipaka ya kumfunza matendo yake na tabia zake, basi hapo haishangazi kwetu kuuona mpasuko ulioko sasa katika familia nyingi isipokuwa zile zilizo rehemewa na Mola. Baada ya nyuma kuwalea vijana wetu kutumia ujana wake kabla ya uzee wake, afya yake kabla ya maradhi yake na kufanya kwake bidii na kumsukuma katika ujana wake kupata (ujira) anapokuwa uzeeni na kuzunguka pamoja na gurudumu linalo saga la Uislamu, kunywa kutoka katika chemichemi ya elimu na kuongeza kupata kwake sifa na akhlaqi njema, baada ya hapo, tumekuja kuwafanya vijana kama yule anaye pitia mauti… Kijana yuko nyumbani kimwili tu lakini kiroho na kihisia hayuko, anaishi mbali na mnara wake halisi. Na hivyo kauli ya mshairi ikawa hakika:

Watu wamekufa lakini sifa zao zingali hai

Na watu wanaishi lakini ni miongoni mwa wafu

Vyombo vya habari na vituo vyake ni silaha iliyo na makali pande zote. Kwa upande mmoja vinafungua fursa kwa mtu na kumwezesha mtu huyo kuwasiliana, kusonga mbele na kunufaika, huku upande mwengine vina elekeza tafakari, ushawishi na tabia ya mtu na kumfanya mtu sponji la kunyonya kila fikra potofu na kila njia iliyo

Endelea Uk..10

pitiliza… Anachorwa akiwa na mbawa pasina kuwa na nguvu yoyote (ya kukataa).

Ili kukabiliana na changamoto hii, ni muhimu kuuregelea na kuufahamu mtazamo wa Kiislamu kwa rika hili. Je, Ahkam zimewafafanua kwa kitu chochote cha kipekee? Na je, kuna msimamo wowote wa kipekee uliochukuliwa kuhusiana nao?

Ili kupambana na uwezo na shinikizo la vyombo hivi vya habari ambavyo vinauchafua utambulisho wa vijana Waislamu, ni lazima kuwe na nguvu imara sawia na zielekee dhidi yake. Inahitaji nguvu ya vyombo vya habari iliyo asisiwa juu ya misingi ya kimfumo inayopinga utenganishaji Dini na maisha, vyombo vya habari vilivyo asisiwa ndani ya upeo wa mpangilio kamili unao yachukulia matatizo ya Waislamu juu ya msingi wa Hukmu ya Shari'ah. Uchafuzi huu wa vyombo vya habari haiwezakani kupambana nao kwa vyombo hafifu vya habari vya Kiislamu vinavyo hutubia makundi maalumu na natija yake havina athari juu ya mujtama. Bali yahitaji mabadiliko ya kimsingi kwa mujtamaa yatakayo regesha mambo kuwa vile yanavyo stahili na kunali mizani ya usawa kati ya Aqeedah ya Ummah huu, thaqafa yake na hotuba za vyombo vya habari zinazo elekezwa kwake. Jambo hili laweza kuonekana kuwa kazi ngumu lakini kinacho lifanya kuwa rahisi ni Uislamu mtukufu kukitwa ndani ya maisha ya Waislamu.

Vyombo vitiifu vya habari vimepata ardhi yenye rutuba na kuwapata vijana wanaoteseka kutokana na utupu wa kifikra na kihisia, wakichukizwa na uhalisia wao na kuwa na kiu ya mabadiliko. Lakini, ni mapinduzi yanayo zunguka katika duara hafifu lisilo badilika… Ni mapinduzi yaliyo kosa lengo kwa hivyo ni muhimu kuangazia juu ya lengo hili ili mambo yaweze kuwekwa sawa… Ni muhimu kuamsha tafakari, kuimarisha utambulisho wa Kiislamu na kumakinisha maana ya ibada kwa Mwenyezi Mungu.

Wacha kilio kipae pambizoni mwetu na wacha kumkumbuka Mwenyezi Mungu kubakie kuzuri zaidi… Subhaanallah Wal-Hamdu Lillah Wa Laa Ilaaha Illallah Wallahu Akbar.

وَالْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ عِندَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَخَيْرٌ أَمَلًا

“Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini” [Al-Kahf: 46].

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ * وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ * وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Ametakasika Mola wako Mlezi Mwenye enzi na yale wanayo mzulia. Na salamu juu ya Mitume. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote” [As-Safaat: 180-182].

**Imeandikwa na**

**Huda Muhammad (Umm Yahya)**

# Msimamo Mpya na Mwamko wa Vijana

**Hotuba ya Nne Katika Kongamano: ‘Vijana Waislamu …Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi’**

السلام عليكم ورحمة الله وبركاته

الحمدُ للهِ الذي هدانا إلى صراطِهِ المستقيم، والسيرِ على هَدْيِ سيدِ المرسَلين.
وَالصَّلاَةُ وَالسَّلاَمُ عَلىَ رَسُوْلِ اللهِ، وَعَلىَ آلـهِ وَأَصْحَابِهِ، وَمَنْ دَعَا بِدَعْوَتِهِ،
وَالْتَزَمَ بِشَرِيْعَتِهِ، وَبَذَلَ جُهْدَهُ لِإِقَامَةِ الْخِلاَفَةِ عَلىَ مِنْهَاجِهِ، وَمَنْ جاَهَدَ فِيْ سَبِيْلِ
اللهِ حَقَّ جِهاَدِهِ. آمين

Rehma za Mwenyezi Mungu (swt) na Baraka zake zitushukie sote, na Allah awajazi kheri kwa kuhudhuria kwenu katika mkao huu.

**Dada zangu, Wahudhuriaji Waheshimiwa, na Wanaharakati Vijana**

Ni lazima tutambue kwamba ukombozi mkubwa umetafutwa na nchi za Kimagharibi dhidi ya watoto na vijana Waislamu nchini Indonesia. Magharibi imekuwa ikiunda mikakati ya kiulimwengu na mipango kadhaa ili kuziteka nyoyo, akili, na utiifu wa vijana Waislamu, ili wawe waaminifu kwa fikra ya usekula, maadili huru, mfumo wa Kimagharibi na nidhamu yake. La kusikitisha, mipango hii inarahisishwa na serikali na kwa sasa inaendelea. Natija yake, msimamo wa vijana Waislamu ulio fafanuliwa na Uislamu, kama waanzilishi wa mabadiliko halisi na walinzi wa Uislamu kwa sasa umetoweka, na uwezo na nishati yao zimepotea.

Mkakati wa Kimagharibi wa kuwafanya huria watoto na vijana Waislamu uko wazi katika waraka “mpango wa kivitendo wa kuzuia misimamo mikali” ulio tabanniwa na Umoja wa Mataifa na kuzinduliwa mnamo Februari iliyopita 12, 2016. Kuna vitu viwili ambavyo twapaswa kuvikashifu. Cha kwanza, kuna juhudi za kuwaweka vijana Waislamu mbali na kuufahamu Uislamu halisi. Cha pili, kuna juhudi za kunyakua uwezo na nishati ya vijana Waislamu ili kuhifadhi utawala wa mataifa ya kirasilimali ya Kimagharibi hususan Amerika – ambayo iko nyuma ya UN.

Juhudi za kuwaweka vijana Waislamu mbali na kuufahamu Uislamu halisi zinajitokeza katika mpango wa kivitendo wa kuwapa vijana uwezo ili kuzuia misimamo mikali. Katibu Mkuu wa UN anataja matunda ya tangazo la vijana jijini Amman mnamo 2015, akisema kuwa vijana wanapaswa kuwa waanzilishi katika uwekaji amani wa kiulimwengu na kuwa wachangamfu katika kuzuia misimamo mikali. Lakini kwa muda mrefu kabla ya hili, Magharibi imebuni hadithi ya kusukuma fikra kuwa wahalifu wa ghasia ni makundi ya Kiislamu. Kuanzia ulipuaji wa majengo ya World Trade Center mnamo 2011 hadi shambulizi la Paris la hivi majuzi, bomu la Ankara, bomu la Sarinah, na ulipuaji wa hivi karibuni zaidi jijini Brussels mwaka huu, wahalifu daima huhusishwa na makundi ya Kiislamu.

Na mkakati wa Kimagharibi wa kupambana na misimamo mikali hauna wasiwasi tena na vita vya kimwili, bali na vita vya kifikra na kisiasa. Kwa pendekezo la shirika la Rand Corporation, Amerika imeunda mtandao wa Waislamu poa kama washirika wake. Zaidi ya hayo, washirika hawa kipaumbele wanajumuisha wasomi Waislamu wa kihuria na wa kisekula, pamoja na wasomi na wanavyuoni vijana wenye misimamo ya kati na kati. Mtafiti mkuu katika kampuni ya Rand Co. Angel Rabasa anawafafanua Waislamu poa kuwa ni wale wanaokubali makundi ya watu wenye matakwa tofauti, utetezi wa wanawake, usawa wa kijinsia, ulinganiaji demokrasia, ubinadamu, na makundi ya kijamii.

**Dada zangu, Wahudhuriaji Waheshimiwa, na Wanaharakati Vijana Rahimakumullah…**

Serikali ya Indonesia kwa sasa imejihusisha na ulinganizi mkubwa wa Uislamu poa ikiangazia vyuo vikuu, shule, na pesantren (shule za mabweni ambazo kitamaduni ni za Kiislamu). Hivi majuzi, Rais Jokowi alimualika sheikh mkuu wa Al-Azhar na kumuomba kueneza mfumo wa Uislamu poa. Fauka ya hayo, serikali hiyo, kupitia Wizara ya Mambo ya Kidini, itabadilisha mtaala wa elimu ya Kiislamu na kutumia jina Uislamu wa amani au Uislamu Rahmatan lil ‘Alamin. Waziri wa Mambo ya Kidini alisema waziwazi kuwa mtaala huu umeandaliwa kwa lengo kuwa wanafunzi watapewa mafunzo ya Uislamu kwa njia ambayo inaheshimu zaidi matabaka ya watu tofauti tofauti, ili kuimarisha usalama na uvumilivu, na kuimarisha demokrasia. Kulingana na yeye, muundo huo pia utakuwa ni njia ya kuzuia kuenea kwa misimamo mikali, ambayo yaweza kuibuka katika taasisi za elimu. Wizara ya Ulinzi inapanga utoaji ushauri wa kitaifa wa ‘ulinzi wa nchi’, hususan kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, na wanafunzi wa pesantren (santri). Inalenga kupanda utaifa katika vijana ili kupambana na fikra za misimamo mikali za kimataifa zinazo ingia nchini humo.

Uislamu poa kimsingi ni itikadi ya kukubali kila kitu kilicho kinyume na mafundisho ya Uislamu. Sio tu kukubali uhalisia wa tofauti, bali ni lazima waikubali fikra yenyewe ya tofauti. Waislamu poa ni wale ambao hawaisumbui jamii ya LGBT na kuwakubali viongozi wa kikafiri kwa jina la haki za kibinadamu; wanafurahika kuhudhuria misa kanisani, na kulegeza msimamo kwa ada za kikafiri kwa jina la makundi ya watu wenye matakwa tofauti tofauti. Hatari ya fikra ya Uislamu poa imedhihirika waziwazi. Shauku jumla imekuwa ikiibuka miongoni mwa Ummah wa Kiislamu. Ummah umegawanywa katika makundi ya Waislamu wenye misimamo mikali na Waislamu poa.

*Endelea Uk..12*

Hakika, vijana Waislamu ni lazima wakuzwe ili wawe na utambulisho halisi wa Kiislamu pamoja na Aqeedah imara ya Kiislamu na akhlaqi njema, pamoja na hamu juu ya matatizo yanayo ukabili Ummah huu. Lakini juhudi hii kwa sasa inalemazwa. Vyama vya wanafunzi Waislamu katika shule, vyuo/vyuo vikuu, na pesantren vinashukiwa kuwa matundu ya magaidi. Natija yake ni, ili kizazi cha vijana kiwekwe mbali na ufahamu sahihi wa Uislamu. Na wabebaji da'wah wenye ikhlasi wanao ng'ang'ana kusimamisha hukmu za Mwenyezi Mungu (swt) wawekwe mbali na Ummah au kutuhumiwa kuwa wenye misimamo mikali. Ukweli ni, Ummah unahitaji Uislamu kisiasa ili kutatua matatizo katika nyanja kadha wa kadha yanayo sababishwa na utabikishaji nidhamu ya kihuria ya kidemokrasia na uchumi wa kirasilimali. Lakini, Magharibi inataka Waislamu kuwa na uadui na Shari'ah na watetezi wake. Magharibi inataka vijana Waislamu – kama wenye uwezo wa kuwa viongozi wa Ummah huu – kuwa Waislamu poa, kwa sababu Waislamu poa hawatatishia uwepo wao.

**Dada zangu, Wahudhuriaji Waheshimiwa, na Wanaharakati Vijana Rahimakumullah…**

Kadhia ya pili hatari ni kuwawezesha vijana katika nyanja za kiuchumi na kijamii, ambapo kikweli ni sehemu ya juhudi za Kimagharibi za kuuteka nyara uwezo wa vijana Waislamu. Katika waraka huo huo 'Mpango wa Kivitendo wa Kuzuia Misimamo Mikali', Umoja wa Mataifa umesema kuwa vichocheo vya ghasia – kando na malengo ya kidini – ni kutelekezwa kijamii na ufukara. Ili kuzuia hili, UN imeunda kitendo cha ufuatiliziaji unaolenga vijana juu ya kadhia za elimu, utoaji ujuzi, urahisishaji ajira, mawasiliano ya kistratejia, tovuti, na mitandao ya kijamii.

Katika kadhia ya elimu, mojawapo ya nukta tunazo hitaji kuzieleza ni umuhimu wa vijana kupata nafasi katika vyanzo vya elimu ya kiufundi na kulea talanta ya ujasiriamali. Muundo wa nidhamu ya elimu ya kirasilimali ni wa kivitendo na unaoendana na masoko; haulengi tena kuzalisha wanasayansi bali kuzalisha wafanyikazi. Wahitimu wa shule za kiufundi, diploma na shahada wametayarishwa kuwa wafanyikazi wa makampuni ya warasilimali wa Kimagharibi. Mwelekeo wa utafiti katika vyuo vikuu hauelekezwi tena na dola katika kujenga uchumi huru wa taifa bali unaelekezwa katika maslahi ya kampuni. Na kiukweli, tatizo la umasikini lenyewe kihakika limesababishwa na utekelezwaji wa nidhamu ya kilafi ya kiuchumi ya kirasilimali.

Katika kadhia ya mawasiliano, tovuti na mitandao ya kijamii, kwa kisingizio kuwa huduma hizi zimetumiwa na wenye misimamo mikali kueneza mfumo wa ghasia na wameweza kusajili vijana, UN itasaidia maelfu ya wanaharakati na wasanii vijana kote ulimwenguni katika kupambana dhidi ya misimamo mikali kwa kutumia vyombo vya habari vya mtandaoni kupitia muziki, sanaa, filamu, vikaragosi, na vichekesho. Wakati huo huo twajua kuwa katika karne iliyopita ni nchi za Kimagharibi ndizo zilizo ongoza uvumbuzi katika teknolojia ya habari na mawasiliano. Wameifanya teknolojia hii chombo cha upandaji thaqafa ya kihuria. Kupitia kupigia debe muondoko wa kimuozo, wa kimada, wa kiutumizi, wa kibinafsi, na wa uhuru wa kimaisha, wamewaangamiza vijana Waislamu.

Katika zama za leo za uchumi uliojengwa kwa msingi wa elimu, kampuni za kirasilimali zinazo tengeza ala za mawasiliano na teknolojia ya habari za kidijitali zinazo tumiwa, zilinufaika pakubwa kutokana na kutumika kwake kwa kuvuna faida kubwa, sera ya moja kwa moja. Ruwaza ya Jokowi ya Indonesia kama soko kubwa kwa uchumi wa kidijitali Kaskazini Mashariki mwa Asia, linalo lenga dolari bilioni 130 mnamo 2020, limemfanya kuwataka Mawaziri wake kudumisha mahusiano mazuri na Bonde la Silicon, kitovu cha sekta ya ubunifu nchini Amerika. Lakini, ni nani haswa anaye likalia bonde hilo, aghalabu likiitwa 'bonde la matumaini'? si mwengine isipokuwa kampuni za kiteknolojia zinazo pigia debe muondoko wao wa kimaisha wa kihuria.

Vyombo vya habari vimewaburuza watoto Waislamu na matineja. Wakati wao mwingi hutumika kujadidisha 'status' zisizo kuwa na maana, 'kuchat' na marafiki hususan wa jinsia ya pili, kuzungumza umbea kuhusu muondoko wa kimaisha wa msanii ambaye ni kiigizo chao. Fikra ya ofa ya kuvutia katika biashara ya burudani; au njia ya haraka ya kupata utajiri kupitia kuwa muigizaji wa kike au muimbaji, imewafanya watoto na vijana Waislamu kuwa tayari kusimama katika foleni ndefu wakati wa hali ya anga ya joto na baridi kwa ajili ya usajili wa matukio kadha wa kadha ya talanta. Bila ya kutaja vipindi vya kuendelea vilivyokuza muondoko muovu wa kimaisha na msimamo huru wa wazazi na watoto, ambavyo vimewafundisha watoto kutowaheshimu wazazi wao na kuunda mitazamo kinyume na akhlaqi za Uislamu.

Huu ndio mkakati wa kiulimwengu na ajenda ya Kimagharibi ya kuviweka mbali vizazi vya Waislamu kutokana na Uislamu halisi na kuuteka nyara uwezo wao. Wamekuwa ni mabalozi wa uhuria na wakati huo huo waathiriwa wa maadili na miondoko ya kimaisha ya Kimagharibi pamoja na nidhamu zake. Vijana wanao usoma Uislamu kwa hamu wanaelekezwa kuwa Waislamu poa kwa manufaa ya fikra, maadili, na nidhamu za Kimagharibi. Huku wengine wakielekezwa kuwa kizazi cha 'alay' kinacho ugua migogoro ya utambulisho, na mustakbali wao umeangamizwa kupitia fikra ya uhuru ya kutenda wapendavyo. Na hivyo wanaporomoka katika giza la ulimwengu, kujihusisha na mihadarati, uzinifu, unywaji pombe, ukahaba, na tabia nyenginezo potofu.

Kwa hakika kupitia mbinu hizi, tumepoteza hazina yetu ya thamani. Na tunaona kuwa imenyakuliwa na mabepari wanao chukia kheri ya Ummah huu. Tunapaswa

***Endelea Uk..13***

kuwaokoa, kwani huu ni upotovu wa kihakika. Mtume Muhammad (saw) asema:

«مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ
فَبِقَلْبِهِ، وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ»

"Yeyote atakaye uona uovu miongoni mwenu, basi na aubadilishe kwa mkono wake; na ikiwa hawezi basi kwa ulimi wake; na ikiwa hawezi basi kwa moyo wake -– na huo ni udhaifu wa imani." [Imesimuliwa na Muslim] Hili ni jukumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) juu yetu. Kuondoa munkar na kutafuta kuregesha msimamo na dori ya vijana kama inavyo takikana na Uislamu. ni lazima wawe viongozi wa mabadiliko, walinzi waaminiwa wa Uislamu. Kama pale Mtume (saw) alipokabiliwa na changamoto za da'wah kutoka kwa Maqureish, vijana ndio waliokuwa safu ya mbele ya wanajeshi walio jihami dhidi ya ukafiri. Vijana ni lazima wawe mabalozi wa Uislamu kama wanavyo onyeshwa na Mus'ab bin Umair (ra), aliyeagizwa na Mtume (saw) kuibeba da'wah hadi Yathrib na hivyo akawa balozi wa kwanza wa Kiislamu. Mus'ab aliachana na fahari yake bandia katika dunia na kuibadilisha kwa izza ya kikweli ya Akhera. Na kwa sababu ya mvutano huu, kwa muda chini ya mwaka mmoja takriban watu wote wa Yahthrib walikuwa wamesilimu, Masha Allah... Allahu Akbar.

Ili kuregesha msimamo, uwezo, na nishati hii ya watoto na vijana Waislamu, ni lazima kuwepo na harakati inayo bebwa na chama cha kisiasa cha Kiislamu ili kunyanyua utambuzi wa vijana Waislamu. Endapo haita bebwa na chama cha kisiasa cha Kiislamu kilicho jengwa juu ya msingi wa mfumo (mabda) – fikra na njia – wa Uislamu, basi lengo la kuregesha msimamo na nishati ya vijana Waislamu kuambatana na Uislamu halita patikana. Litapatikana pekee kwa chama cha kisiasa cha Kiislamu kitakacho fichua njama ya Kimagharibi ya kuangamiza kizazi kichanga cha Uislamu, na kufichua kufeli kwa mfumo wa kisekula wa kirasilimali na demokrasia huru ambayo imesababisha mateso tu pekee katika maisha ya wanadamu.

Hakika, dori hii muhimu ya vijana itaimarishwa tu ndani ya mujtama unaotekeleza Uislamu wote (kaaffah). Ni Khilafah kwa njia ya Utume ndiyo itatayarisha kila kitu kinacho hitajika kwa ajili ya kuwawezesha vijana. Nidhamu za kielimu, kijamii, kiuchumi na kisiasa zinazo tekelezwa na Khalifah zote zitasaidia kupatikana kwa uwezo wa vijana kama walinzi waaminiwa na watetezi wa Uislamu, ambao utaleta maendeleo katika hadhara ya ulimwengu na kuhifadhi maslahi ya Ummah. Akili na nyoyo zao daima zitafungamanishwa na Uislamu na izza ya Ummah. Hivyo basi, mwelekeo wa leo wa uimarishaji fikra na uwezeshaji vijana Waislamu unalenga kusimamisha Khilafah 'ala Minhajin Nubuwwah.

Hatimaye, nawalingania vijana Waislamu kwa neno la Mwenyezi Mungu (swt) katika Surah Kahf ayah 28:

وَاصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ وَلَا تَعْدُ
عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ
هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا

"Na isubirishe nafsi yako pamoja na wale wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimtii tuliye mghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamanio yake yakawa yamepita mipaka."

والحمد لله رب العالمينوالسلام عليكم ورحمة الله وبركاته

**Imeandikwa na**

**Umm Fadhiilah - Indonesia**

# Kukabiliana na Mgogoro wa Kitambulisho cha Vijana wa Kiislamu

**Hotuba ya Tano Katika Kongamano: 'Vijana Waislamu …Waanzilishi wa Mabadiliko Msingi'**

Assalamu alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu

**(1) Utangulizi:**

Dada zangu wapendwa na wageni waheshimiwa, mgogoro wa utambulisho unaoathiri wengi wa vijana wetu wa Kiislamu ni mojawapo ya kadhia sugu mno zenye kuathiri Ummah huu. Na kama ulivyo mgogoro wowote, kukabiliana nao vilivyo na kwa haraka ni wajib. Ni wajib kwani ndiyo itakayoamua mafanikio ya watoto wetu na sisi wenyewe katika maisha haya na maisha ya kesho. Na ni wajib kwani ndio kitovu cha mafanikio ya mustakbali wa Ummah huu na hadhi ya Dini yetu hapa ulimwenguni.

Dada zangu, mwanachuoni mkubwa wa Kiislamu, Imam Ghazali (RH) wakati mmoja alisema, "Mtoto ni amana mikononi mwa wazazi wake. Na moyo wake msafi ni kito cha thamani kisichokuwa dosari, kisichokuwa na mchongo au umbile lolote. Hukubali kuchongwa na kufinyangwa katika mwelekeo wowote. Endapo atalelewa na kufunzwa uzuri, atakulia juu ya hili. Mtoto aina hii atafanikiwa hapa duniani na kesho Akhera na wazazi, walimu na wakufunzi wake wote watashirikiana katika malipo haya. Lakini endapo mtoto huyu atalelewa katika uovu na utepetevu, atageuka kuwa msiba na kutumbukia katika maangamivu, na wanao husika na ulezi wake watashirikiana katika dhambi lake. Endapo atakulia katika uovu na kuachwa bila ya kukanywa, atageuka kuwa msiba na ataangamia."
Dada zangu, kwa kweli nyoyo za watoto wetu wanapokuwa wadogo huwa ni safi, zisizo chakachuliwa, mithili ya kito cha thamani. Endapo watazamishwa ndani ya Dini kwa njia sahihi, na kuitambua Haki na kheri inayo tiririka kutokana nayo basi insha Allah watakuwa vijana ambao nyoyo zao ziko imara juu ya haki, wenye yakini na Imani zao za Kiislamu, wenye kujitolea juu ya majukumu yao ya Kiislamu, mashujaa katika kuzungumza Dini yao na dhidi ya batili na dhulma na wenye mapenzi kwa uongofu na kuchukia yale ambayo Mola wao (swt) ameyataja kuwa ufisadi, uchafu, na dhulma. Watakuwa ndio chimbuko la kheri kwa familia zao, jamii zao, mujtama zao, na Ummah huu. Na watakuwa ndio wenye kudhihirisha sifa za kuleta mageuzi ya kweli hapa ulimwenguni, wakibeba majukumu mabegani mwao na kuwezeshwa kwa suluhisho sahihi la Kiislamu la kuuinua Ummah huu na kihakika ulimwengu huu kutokana na matatizo yasiyo idadi na dhulma inayo ukabili leo.

Lakini lengo hili tutalifikiaje? Vipi tutajenga na kuhifadhi utambulisho wa Kiislamu katika vijana wetu na kuwatayarisha kupambana na changamoto kuu wanazo zikabili katika kushikamana na Dini yao, kuzungumza Dini yao, na kung'ang'ana kwa ajili ya Dini yao?

Leo, ningependa kuzungumzia baadhi ya nukta muhimu na baadhi ya fahamu msingi ambazo zahitaji kujengwa ndani ya vijana wetu ambazo bila shaka ni muhimu mno katika kukabiliana na mgogoro huu wa utambulisho, na kuwawezesha ili kuzishinda changamoto wanazo kumbana nazo barabara insha Allah.

Lakini dada zangu, kwanza kuna swali ambalo ni lazima tulijibu wenyewe – kama wazazi, jamii, na kama Ummah – ikiwa tunataka kukabiliana barabara na mgogoro huu wa utambulisho wa vijana wetu. Nalo ni –tunataka nini haswa kwa watoto wetu? Je, tunauona Uislamu na Uislamu pekee katika nyanja zake zote – kiroho, kiakhlaqi, kijamii, na kisiasa kama njia pekee ya kuwaokoa watoto wetu kutokana na matatizo yanayo umiza roho ambayo vijana wengi wanakumbana nayo leo; njia pekee ya kuwawezesha kutoa mchango wenye natija ya kikweli kwa maendeleo ya wanadamu na hali bora ya ulimwengu huu, pamoja na kuwadhamini mafanikio msingi katika maisha haya na maisha yajayo?

• AU kuna maadili, fikra, tamaduni nyingine ambazo hazikujengwa juu ya Uislamu ambazo tunaunda kwazo mitazamo, matendo, misimamo juu ya mafanikio na matarajio yetu na ya watoto wetu ambazo zinatusababishia kulegeza msimamo kwa Dini yetu, tukisababisha mchanganyiko wa jumbe na mkanganyiko machoni mwa vijana wetu, na hata chuki akilini mwao dhidi ya Uislamu?

• Vipi kwa mfano, tunaweza kutarajia watoto wetu kuepukana na mahusiano nje ya ndoa, ikiwa tunaruhusu tamthilia, filamu na muziki zinazo pigia debe, kuvutia na kuhamasisha kuhusu uchafu wa mahusiano hayo kuingia ndani ya sebule zetu, au ikiwa tunaruhusu mchanganyiko huru wa wanaume na wanawake katika mijumuiko yetu ya kijamii na harusi kinyume na Uislamu?

• Vipi tutaweza kujenga uhahamu (aqliyya) katika vijana wetu kuwa mafanikio makuu ni kupata Radhi za Mola wetu na kuingia mabustani ya Pepo, ikiwa tunawaruhusu kulegeza msimamo katika swala zao, vazi lao la Kiislamu na majukumu mengineyo ili wafaulu katika elimu au kutafuta ajira au kazi ya kiwango cha juu, ikiwapelekea wao kuamini kuwa kilicho muhimu ni cheo, utajiri na kupata vitu vya kidunia?

• Vipi tutaweza kuwalea vijana wetu kushikamana na matarajio ya Mwenyezi Mungu (swt), ikiwa matarajio yetu ya namna wanavyo vaa, namna ya tabia zao,

*Endelea Uk..15*

nani wanaye oana, utiifu wao, mitazamo yao ya kisiasa yamejengwa juu ya maadili yasiyo ya Kiislamu, mila, utaifa, nidhamu ya kidemokrasia iliyotungwa na mwanadamu au matarajio yaliyosemwa na familia au jamii, badala ya lile analo amuru Mwenyezi Mungu (swt)?

• Na vipi tutawapa motisha vijana wetu kuwa mashujaa na kusimama kwa ajili ya Uislamu ikiwa tuna hofu ya kuwashajiisha kuzungumza kwa ajili ya Ummah wao nchini Palestina, Syria na kote ulimwenguni, au dhidi ya mashambulizi juu ya kipenzi chetu Mtume (saw) na Dini, au dhidi ya vita na madhalimu wa Kimagharibi katika ulimwengu wa Waislamu, au katika kuunga mkono Shari'ah au Nidhamu ya Mwenyezi Mungu – Khilafah – kwa kuogopa kuwa watatazamwa kama wenye misimamo mikali na kuwekwa chini ya rada za serikali dhalimu.

• Dada zangu wapendwa, endapo tutawasilisha jumbe za mkanganyiko na kuwa na misimamo miwili miwili kwa vijana wetu kupitia mitazamo, maneno na matendo yetu wenyewe, kamwe hatutaweza kukabiliana barabara na mgogoro wa utambulisho wanaokumbana nao. Hivyo basi, hatua ya kwanza ya kuwaokoa watoto wetu ni kutathmini upya utambulisho wetu wenyewe na kudumu kwetu katika kushikamana na Dini yetu.

**(2) Kujenga Itikadi (Aqeedah) kwa Kukinai:**

• Baada ya kuelezea nukta hii muhimu ya mwanzo, dada zangu, ni hatua gani muhimu nyenginezo ambazo twahitaji kuchukua ili kukabiliana na mgogoro wa utambulisho katika vijana wetu?

• Kwanza dada zangu, mojawapo ya zawadi za thamani mno ambazo twaweza kuwapa watoto wetu ni uwezo wao wa kutafakari wenyewe kuhusu maisha na ulimwengu, kwa njia ambayo wataweza kutofautisha haki kutokana na batili. Hii yamaanisha kwanza, kuwawezesha kujenga ukweli wa Itikadi ya Kiislamu kwa kukinai kuliko katikiwa kupitia kuwapa dalili nzito za kiakili zinazo jenga yakini ya kuwepo kwa Muumba na kwamba Qur'an ni maneno Yake kwa asilimia 100 – kama alivyo sema Mwenyezi Mungu (swt),

إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمۡ يَرۡتَابُو

"Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa..." [Al-Hujraat: 15].

• Katika ulimwengu wa leo dada zangu, ambamo vijana wetu wanashambuliwa kwa hotuba katika vyombo vya habari au mitandaoni za kuupinga Uislamu, kushambulia Imani zake, kujenga hofu katika utekelezaji Uislamu, na lile dai kuwa Imani kwa Mungu na dini haingii akilini, iliyopitwa na wakati, ni ya watu wenye akili finyo pekee – kujenga Aqeedah ya Kiislamu kwa kukinai kiakili kuliko katikiwa ni nyeti mno. Ni hili ndilo litakalo badilisha Uislamu kutoka kuwa ni kitu ambacho vijana wengi wanakitazama kama walicho rithi tu kutoka kwa wazazi wao, hadi kuwa ni kitu walicho kikinai kiakili kuwa na majibu sahihi ya maisha na hivyo kinapaswa kupangilia fikra na matendo yao.

• Ni yakini hii katika Imani ndiyo itakayo fanya Pepo (Jannah) na Moto (Jahannam) kuwa uhalisia usio badilika machoni mwa vijana wetu inshaAllah, na kuhisabiwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni fahamu nzito akilini mwao, ikiwapelekea kuishi maisha yao kwa mujibu wa Sheria na Mipaka yake (swt) inshaAllah. NA ni yakini hii katika Imani ambayo pia itajenga ufahamu safi inshaAllah kuwa lengo maishani na mtazamo sahihi wa mafanikio sio kutafuta vyeo vikubwa na starehe fupi za maisha haya, au kukubaliwa na kupata umaarufu miongoni mwa marafiki na mujtama bali ni kupata Radhi za Mwenyezi Mungu (swt) na thawabu zisizo kifani kesho Akhera.

• Hakika dada zangu, katika ulimwengu ulio pagawa na matumizi ya kimada unaojaribu kuwaundia vijana wetu Pepo duniani kwa matamanio na starehe nyingi za kuvutia zinazo kwenda kinyume na Dini yao, au ambapo utafutaji wa mali za dunia hii – simu, kifaa, ala, nguo za kisasa – zimetawala wakati na umakinifu wao – ni muhimu mno tujenge ndani ya vijana wetu hamu ya Pepo inayo wanyanyua juu ya starere fupi za dunia hii na kuwawezesha kuzikubali hukmu za Kiislamu zilizo wekwa juu ya maisha yao – kupitia kudumu kuwakumbusha kuwa zote hizi si chochote isipokuwa ni tone ndani ya bahari ikilinganishwa na starehe zisizo kifani zinazomsubiri kijana mwema Peponi – kama Mtume (saw) alivyosema,

وَاللَّهِ مَا الدُّنْيَا فِي الآخِرَةِ إِلاَّ مِثْلُ مَا يَجْعَلُ أَحَدُكُمْ إِصْبَعَهُ هَذِهِ - وَأَشَارَ يَحْيَى بِالسَّبَّابَةِ - فِي الْيَمِّ فَلْيَنْظُرْ بِمَ يَرْجِعُ

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu, haikuwa dunia kwa Akhera isipokuwa ni mithili ya mmoja wenu kutia kidole chake hiki – na akaashiria kwa kidole cha shahada – ndani ya bahari kisha aangalie atakacho baki nacho kidoleni hicho."

• Dada zangu wapendwa, ni kukinai huku katika Aqeedah na kuwa na hamu ya Pepo ndio yaliyo mpelekea kijana mchungaji dhaifu Abdullah ibn Masud (ra) kuwasomea Qur'an Maquraysh, akijua kwamba watampiga; ndiko kuliko mpelekea kijana Jafar ibn Abi Twalib (ra) kuzungumza kwa niaba ya Waislamu katika mahakama ya Mfalme wa Habasha, bila ya kutishwa na uwepo wa watu walio na ufasaha zaidi katika Maquraysh walio tumwa kuzungumza dhidi ya waumini. Na dada zangu, ni kukinai huku ndiko ambako inshaAllah kutawajaza vijana wetu ushujaa wa kushikamana na Imani zao za Kiislamu katika hali yoyote ile; kusimama dhidi ya shinikizo la wandani wao, hawahofii kubandikwa majina au kuwa tofauti na marafiki zao au hata kubaguliwa kutokana na vazi lao, matendo yao au rai zao za Kiislamu, na kuzungumza kwa ajili ya Uislamu pindi unapo shambuliwa.

*Endelea Uk..16*

**(3) Kuvunja Kivutio cha Mfumo Huru wa Kisekula wa Kimaisha:**

• Hatua ya pili ya kukabiliana na mgogoro huu wa utambulisho katika vijana wetu, dada zangu, ni kujenga njia ya kutafakari kwa kudadisi ndani yao inayo wawezesha kutenganisha uongo kutokana na ukweli kuhusiana na fikra zilizo tawala na simulizi zinazo washambulia kutoka katika vyombo vya habari au mujtama na kupambana nazo kwa hekima. Kuwawezesha kupuuzilia mbali uongo dhidi ya Uislamu na kuvunja kivutio cha mfumo huru wa kisekula wa kimaisha ni muhimu mno katika wakati ambao vijana wetu wanafanywa wahisi kuwa Uislamu ndio chanzo cha matatizo yao mengi na ghasia duniani, na kwamba mfumo huru wa kimaisha wa Kimagharibi ndio njia ya furaha na mafanikio, na ustawi na ufanisi katika hii dunia.

• Twahitaji kuwaonyesha – kuwa Uislamu sio uliosababisha janga la mihadarati, ulevi, usumbufu, magenge, uhalifu wa bunduki na tabia nyingine za kiuhalifu zilizo waathiri vijana leo bali ni maadili huria yanayo pigia debe muondoko wa kimaisha wa starehe za kibinafsi na kufuata matamanio ya mtu bila ya kujali matokeo. Uislamu sio uliovunja haiba na Imani ya wasichana wengi wadogo kwa sababu hawawezi kujilinganisha na muonekano wa wasanii na viigizo wengine bali ni muundo wa urembo wa Kimagharibi usio wa kihakika ambao umenasibishwa na mafanikio. Uislamu sio unao wafanya vijana wengi kuhisi kufeli au kuchukuliwa kama walio laaniwa wanapo shindwa kudumu katika fesheni za simu au bidhaa bali ni thaqafa ya kimada ya kirasilimali inayo sawazisha thamani ya mtu binafsi na mali za kidunia. Sheria za kijamii za Kiislamu sizo zilizo unda mila ya utovu wa heshima kwa wasichana na wanawake, ikipelekea ghasia na dhulma za kijinsia bali ni mujtama zinazo tukuza uhuru wa kijinsia na kuruhusu hadhi ya wanawake kudunishwa kupitia kuwafanya kuwa vyombo vya ngono katika sekta ya burudani na unadi bidhaa. Na Uislamu sio ulio zalisha umasikini mkubwa na ukosefu wa ajira, ukosefu wa usawa katika utajiri, na huduma duni za elimu na matibabu kote duniani bali ni nidhamu ya sumu ya kirasilimali ndiyo iliyo sambaratisha uchumi, kuzizonga na madeni makubwa yenye riba, na kuwapendelea matajiri kuliko masikini.

• Sambamba na haya dada zangu, pia tunahitaji vijana wetu wafahamu na kuunganisha kwa hekima na dalili kwa wale wanao wazunguka, kuwa sio sura ya kimakosa ya mfumo wa Kiislamu inayo chochea ugaidi bali ni hasira zilizo chochewa na uingiliaji mambo wa Kimagharibi na vita vya kikoloni katika ulimwengu wa Waislamu ambavyo vimeuwa maelfu ya Waislamu. Tunahitaji wao wajadili kwa uwazi kuwa ni Imani hizo hizo za Kiislamu ndizo zinazo wasukuma kutekeleza Uislamu ambazo pia zinawawajibisha kuwaheshimu wazazi na walimu, kuamiliana na wanawake kwa hadhi, kuepuka uhalifu, kutia juhudi kwa ajili ya manufaa ya wanadamu na kupinga ghasia dhidi ya wasiokuwa na hatia au kuwanyanyasa walio katika dini nyingine. Na twahitaji vijana wetu kufahamu na kusema kwa imani kuwa si katika misimamo mikali kuzungumzia kuhusu dhulma za serikali au kuzungumza kwa niaba ya wanyonge, au kulingania Shari'ah ya Kiislamu au Khilafah kutabikishwa katika ardhi zetu ambayo itabadilisha udikteta kwa uangalizi kwa watu, kuzibadilisha dola za kiaskari kwa uwajibikaji na uadilifu katika usimamizi, na ambayo itatumia utajiri wa ardhi zetu kwa ajili ya mahitaji ya watu kuliko kujaza mifuko ya serikali za kigeni, mashirika malafi au kwa kipote cha mabwenyenye wachache.

• Dada zangu, tunahitaji kuwafanya watoto wetu kuchukua umiliki wa midahalo hii na kutawala simulizi kuhusiana na Uislamu na mifumo mingine ya kimaisha ndani ya mujtama zao, wakijihami kwa ukweli.

**(4) Kuufahamu Uislamu kama Dini Iliyo na Suluhisho la Matatizo ya Kimaisha na Kujenga Fahari Katika Thaqafa na Historia ya Kiislamu:**

• Na mwisho dada zangu, katika ulimwengu ambao Uislamu unaonyeshwa kama uliopitwa na wakati, katili, na wenye kukandamiza wanawake na dini nyingine, na kitu cha kihistoria kisicho endana na maisha ya kisasa, ni muhimu mno tuwajenge vijana wetu kuwa na imani katika Dini yao na kuitazama kama inayo endana na maisha yao na ulimwengu huu wa karne hii ya 21, kuliko kuwa ni mkusanyiko tu wa ibada na hukmu. Hili twaweza kulipata pekee kupitia kuwafanya waufahamu Uislamu kama Dini kamilifu iliyo na misingi, sheria na suluhisho kwa matatizo ya kileo ya kimaisha – kiroho, kiakhlaqi, kijamii, kisiasa, kimahakama, kielimu, katika uchumi, na yasiyokuwa haya – kwani Mwenyezi Mungu (swt) asema, **[مَّا فَرَّطْنَا فِى ٱلْكِتَـٰبِ مِن شَىْءٍ]** "Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote..." [Al-Anaam: 38]
Na kwa hili, pia kujenga fahari katika thaqafa na historia ya Kiislamu na yale iliyoleta kwa wanadamu na yale iliyo faulu katika dunia hii ya uadilifu, ufanisi, ustawi, maendeleo ya kisayansi, ubinadamu, kulinda haki za wanawake na dini za wachache, mafanikio ya kiusomi, na nidhamu za elimu na matibabu za kiwango cha juu wakati wa zama za utawala wake juu ya ardhi zetu za Waislamu, chini ya kivuli cha Khilafah tukufu.

• Waonyesheni kuwa ni sheria za nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu ndizo zinazo shikilia ufunguo wa ugavi sawa wa utajiri na uundaji wa uchumi ulio nawiri – kama ilivyo onyeshwa kupitia Khilafah ya Umar bin Abdul Aziz aliye arifiwa na afisa wake nchini Iraq kuwa hata baada ya pesa za dola kutumika kukidhi haja za watu, kulipa madeni yao, kuwasaidia kifedha katika ndoa zao, bado kulisalia pesa katika hazina. Umar kisha akamuagiza kuitumia ziada hii kuwasaidia watu kulima ardhi zao. Subhanallah!

• Twahitaji kuwaonyesha vijana wetu kuwa ni Dini ya

*Endelea Uk..17*



Email: info@uqab.or.ke

Kiislamu pekee ndiyo inayo pinga uhuru wa kijinsia, kuharamisha udhalilishaji na uchukuaji wa wanawake kuwa vyombo vya ngono, na kuasisi mpangilio mpana wa sheria ili kudhibiti mahusiano kati ya wanaume na wanawake ili kuhifadhi hadhi yao, ambayo yaweza kutatua janga la ghasia na unyanyasaji wa kijinsia wa wanawake unao athiri ulimwengu leo.

• Na, twahitaji kuwaonyesha watoto wetu kuwa ni nidhamu ya Kiislamu pekee inayopinga taasubi ya kimada na ya kikabilia katika kushughulikia matatizo ya wanadamu na ambayo inatumikia kwa ikhlasi mahitaji ya wanadamu ndio inayoweza kutatua mgogoro wa wakimbizi – kama ilivyo dhihirishwa kwa vitendo vya Khilafah Uthmaniyya mnamo 1492, pindi Khalifah Bayezid wa pili alipotuma msafara wake wote wa majeshi kwenda kuwaokoa Mayahudi 150,000 wa Ulaya waliokuwa wakiteswa na Wakristo wakati wa Uchunguzi wa Kihispania na kuwakaribisha katika ardhi za Khilafah na kuamiliana nao kwa usawa kama raia, na kuwaruhusu kujiimarisha.

• Dada zangu, ni kwa kujenga fahari hii katika thaqafa na historia ya Kiislamu ndani ya vijana wetu, na kuufahamu Uislamu kama Dini pana iliyo na suluhisho kwa matatizo yote ya wanadamu katika zama zote na mahali popote ndio itakayo wawezesha kupambana na mashambulizi dhidi ya Dini yao, kupinga ajenda ya Kimagharibi ya kuupa sura mpya Uislamu, kukuza ndani yao imani katika utambulisho wao wa Kiislamu, na kuwawezesha kuzungumza kwa ajili ya Uislamu kwa hekima na kauli thabiti.

• Lakini fauka ya hayo, dada zangu, ni katika kutambua maumbile halisi ya Uislamu ndiyo yatakayo jenga ndani ya vijana wetu hisia kubwa ya majukumu mbele ya Ummah huu na hakika mbele ya wanadamu baada ya kutambua nguvu kubwa iliyopo mikononi mwao ya kuleta mabadiliko halisi katika ulimwengu huu kupitia Dini hii, ikiwapatia sababu stahiki ya kung'ang'ania ambayo kihakika yaweza kujenga mustakbali bora wa ardhi zao na ulimwengu huu, ikiwemo kudhamini matarajio yao ya kielimu na kiuchumi; sababu ambayo haitapoteza nguvu zao, kusaliti matumaini yao, na kuzima ari yao, wala si sababu ambayo itawahusisha katika ghasia tasa kama njia ya mabadiliko ya kisiasa bali vita vya kifikra ili kusimamisha Dini hii katika utawala, kwa kufuata Sunnah ya Mtume (saw).

• Dada zangu wapendwa, yote haya ndio yatakayo wajenga vijana wetu wa Kiislamu kuwa "Waanzilishi wa mabadiliko halisi", wakiwezeshwa kwa Uislamu, ukiunganishwa na hamu na nguvu nyingi ambazo vijana wetu wanazo katika kuleta tofauti halisi hapa ulimwenguni lakini kwa njia inayo wapatia Radhi za Mola wao na kuwadhamini malipo makubwa kesho Akhera. Na ni kupitia kuwalea vijana wetu kusimama kwa changamoto hii kuu ndio pia inshaAllah itarahisisha kurudi kwa haraka kwa dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, ambayo dada zangu ndio uongozi utakao hudumikia kama mlinzi wa kweli wa utambulisho wa Kiislamu wa watoto wetu – dola itakayo wazamisha ndani ya maadili matukufu ya Kiislamu na kuzalisha mazingira ambayo daima yatawakumbusha kuhisabiwa kwao na Mwenyezi Mungu na umuhimu wa kujitolea kwa ajili ya Akhera, dola ambayo vyombo vyake vya habari na nidhamu yake ya elimu zitakuza maadili na matendo mema, kukuza uchaMungu (Taqwa) wa vijana wetu na mapenzi yao kwa Dini yao. Itaunda vijana wengi walio na utambulisho wa kipekee wa Kiislamu watakao dhihirisha tabia zao tukufu na waja wa Mwenyezi Mungu wenye kujitolea, kubeba mizigo ya Ummah wao mabegani mwao, wapinzani wakali wa dhulma, na wenye kuwakilisha sifa za viongozi wa wanadamu.

• Dada zangu, vita vya kulinda utambulisho wa Kiislamu wa kizazi chetu kijacho kamwe havitashindwa pasina kusimamishwa kwa haraka nidhamu hii – Khilafah kwa njia ya Utume. Kwa hivyo kuongezea juu ya ujenzi wa fahamu za Kiislamu ndani ya vijana wetu leo, pia vile vile tutulize makini yetu na kutia juhudi zetu katika kuregesha dola hii tukufu katika ardhi zetu na kupitia kwayo kuunda kizazi cha vijana ambacho ndicho chanzo cha fahari kwa Ummah huu na ambao wanasimama kama mfano na chanzo cha matarajio kwa vijana wa ulimwengu huu.

Mwenyezi Mungu (swt) asema, **[وَرِضۡوَٰنٞ مِّنَ ٱللَّهِ أَكۡبَرُۚ ذَٰلِكَ هُوَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ]** "...na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote. Huko ndiko kufuzu kukubwa." [At-Taubah: 72]

**Imeandikwa na**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Tahadhari ya Kijana Muislamu Mwanzilishi wa Mabadiliko Halisi

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Bwana wa Walimwengu, na swala na salamu zimshukie Mtume Mtukufu Mteule na familia yake, maswahaba zake na wale wanaomfuata kwa ihsani hadi Siku ya Malipo. Mola wetu, tusamehe dhambi zetu, tupe afueni kutokana na mitihani yetu, tulinde na hofu zetu na tujaaliye miongoni mwa waja wako watakatifu na wenye ikhlasi; ambao hawakiuki mipaka wala kudhulumu. Mola wangu, nifungue kifua changu, na unifanyie wepesi jambo langu, na ufungue fundo katika ulimi wangu na kauli yangu ifahamike.

Dada zangu waheshimiwa, nawaamkua kwa maamkizi ya Uislamu, As-Salaamu Alaikunna Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuhu, jumuiko lenu na kukusanyika kwenu huku kubarikiwe na natoa shukrani zangu kwa kila mmoja aliye itikia mwaliko huu na kila aliye chukua nafasi ya kufanikisha mkutano huu…

Vijana wanawakilisha dhihirisho la nishati na ubunifu, ni kichwa cha utoaji na kilicho chonjo. Lakini, vijana wanateseka leo kutokana na uhalisia mchungu na wakuhuzunisha, usimamizi mbaya na kutelekezwa, na kutokana na ukosefu wa uwakilishi wa matarajio yao kama vijana Waislamu wanaotaraji kuregesha ubwana wao, ardhi yao iliyo nyakuliwa na rasilimali zilizo fujwa.

Mkoloni amefanya kazi kwa takriban karne moja kumtia umagharibi kijana wa Kiislamu, ili kumfanya awe na shaka na kukinai kwake na utambulisho wake. Na mkoloni huyu aliivunja Khilafah na kuchagua kikundi kukielimisha na kukilea kwa fahamu za kimagharibi. Kisha wakakitumia kushambulia Uislamu na kulingania ukombozi kutokana na fahamu zote ambazo Ummah umelelewa na kuelimishwa nazo. Hii ni ikiongezewa na kujisalimisha kwa fikra kuwa maendeleo na ufanisi kamwe hayawezi kutokea isipokuwa turathi jumla ya kifikra ya Kiislamu ishambuliwe na ikifuatiwa na kuikimbilia hadhara ya kimagharibi pamoja na viungo vyake vyote. Na hivyo basi vijana wakachanganyikiwa na fikra hizi zenye sumu zilizo legeza ghariza zake na kuvifanya vipimo vyake kuwa kupata maslahi huku akiondoa Aqeedah ya Kiislamu kuwa msingi wa fikra yake. Hii ilisababisha kuyumba kwa utambulisho (shakhsiya) wa kijana Muislamu ambapo hamasa zake zingeamshwa kupitia miito duni, kama vile uhuru miongoni mwa mengineyo, na kuzalisha vitambulisho visivyokuwa na utulivu. Kisha serikali zilizoko mamlakani zilitenganishwa kutokana na majukumu yote kwa madai kuwa vitambulisho hivi vilikuwa ni natija ya kimaumbile ya mabadiliko ya kimwili ambao waliuita umri wa ubarobaro au utineja. Wanabeba lawama kwa kufeli kwao kiakili katika rika hili na fikra zao, ambapo imesababisha mateso na msongo wa mawazo.

Na hili wala si geni kwa yule aliyecheza kamari kwa kuushambulia Ummah wa Kiislamu ili kujibunia cheo chake miongoni mwa mataifa. Si geni kwa juhudi za papatiko kufanywa ili kupata lengo lake. Hii hapa ni miongoni mwa taarifa zilizo chaguliwa zinazo ashiria nia za wakoloni: "Kikombe na msichana mrembo vinafanya kazi pamoja kuuangusha Ummah wa Muhammad zaidi kuliko vile ambavyo bunduki zingefanya". Na hivyo basi wamezificha ndani ya mapenzi kwa mali za kimada na matamanio.

Na pindi Magharibi ilipopata dhamana kutoka kwa serikali hizo kuwa zimezika shingoni mwa Waislamu ambao wanabeba ajenda zao, waliridhika na makao (waliyopewa) ili kuwatelekeza vijana ndani ya mpangilio fisidifu wa elimu, muundo mbovu wa kiuchumi na muundo uliofeli wa kiutumwa wa kisiasa. Vijana hatimaye walijipata ndani ya hali ya mateso wasijue jinsi ya kujitoa kutokana nayo.

Wakati huo huo, katika miongoni mwa Mashabab kuna kikundi kibunifu ambacho wakoloni wanaridhika kukiruhusu kuhamia nchi zao na kuwafanyisha kazi ndani ya maabara zao. Tutawasilisha baadhi ya takwimu kama mfano mdogo wa uhalisia huu. Kwa mujibu wa Shirikisho la Kiarabu, asilimia 50 ya madaktari na asilimia 23 ya wahandisi kutoka maeneo jumla ya Kiarabu huelekea Ulaya huku asilimia 54 ya wanao kwenda huko kusoma hawarudi nchini mwao. Na kutokana na ripoti ya serikali kuhusu uhamiaji katika mwaka wa 2012, wanafunzi elfu 57 kutoka Tunisia huhamia nchi za kigeni huku kiwango cha wanaorudi kikiwa si zaidi ya asilimia 10. Idadi ya wafanyi kazi wanaohamia kutoka Tunisia ikiwa ni 83,529, huku pia ikitajwa katika ripoti nyengine kupitia Idara ya Makao na sera za Uhamiaji katika Chuo Kikuu cha Arab kuwa Waarabu hupoteza dolari bilioni 1.57 kila mwaka kutokana na uhamaji wa akili au mabongo.

Na katika vijana ni wale wanaojipata wamekwama katikati ya lindi la ukosefu wa ajira, uhalifu na uhamiaji huku wakiokoka kutoka katika janga moja na kutumbukia katika janga jengine ambalo hata ni baya zaidi. Hiyo ni kwa sababu Magharibi imetabanni sera yake ya kutoa makao na kufurusha kwa mujibu wa mahitaji yake.

Katika kiwango cha Maghribi (yaani Morocco, Algeria na Tunisia), idadi ya vijana inafikia takriban nusu ya wakaazi. Wengi wao wako nje ya soko la ajira na wengi wao wangali waseja na wanawategemea baba zao kusimamia mahitaji yao ya kimaisha. Na inashangaza kuwa katika kila eneo kuna wizara inayoitwa 'Wizara ya Vijana' lakini ambacho hakishangazi ni kuwa wizara hizo hazijaleta manufaa yoyote, na hiyo ni kwa sababu ndio sifa yao kutoa sura isiyo na thamani ya kihakika.

Ama kuhusu taasisi za kielimu, zinawakilisha nafasi wazi ya kuwapiga muhuri vijana kwa maadili na masrufu yao. Zinafanya kazi waziwazi kudhamini uzalishaji wa wawakilishi wanao hudumia maslahi ya wenye ushawishi

*Endelea Uk..19*

ndani ya mujtama na haswa wakoloni na wasaidizi wao. Maalumati ya kielimu yaliyo fafanuliwa katika mipango na mitaala bila ya kusitasita ni feki ingawa kuna wito wa mageuzi, kwa kuwa kimsingi yanazunguka pambizoni mwa mabadiliko bandia kuhusiana na nyakati, nafasi ya shule na mbinu zilizo tabanniwa.

Kwa hivyo Tunisia, kwa mfano, wanadai kuwa wanafanya mabadiliko ya elimu huku wakitumia juhudi na pesa zao kusambaza amali na vilabu vya kithaqafa, kwa mujibu wa kisingizio chao. Lakini ni thaqafa ipi wanayo zungukwa nayo? Michezo inayoitwa ya kiini macho na uchezaji densi wa muziki wa kelele iliyokosa alama za aibu na heshima ambayo yalipaswa kutekelezwa kama thamani muhimu zaidi na kujengwa ndani ya thaqafa ya yule anayekulia. Vipi watawajibika kwa ajili ya mipango ya kielimu wakati ambapo hawajapewa idhini? Hakika, wanasubiri marekebisho kutoka kwa wale walio waajiri.

Ndani ya hali hii mbaya kwa vijana, vyama na mashirika yameendesha usajili, yakitoa wito kwa Mashabab/vijana kuwa kiungo muhimu na chenye athari katika mchakato wa mageuzi kama wanavyouita. Yakisaidiwa kinidhamu na vyombo vya habari kwa hofu kuwa mageuzi msingi na sahihi yatatokea mikononi mwa watoto wa Ummah walio na ikhlasi.

Kuongezea haya ni vyama vya kigeni vinavyo fanya kazi chini ya kichwa “Viongozi wa mustakbali” ambavyo vinawavutia vijana na kuwakuuza kwa thaqafa ya kimagharibi kwa kutumia miundo ya kuvutia. Vinawatafuta wale wanaomiliki sifa za uongozi ili kuwahusisha katika hali za kutatanisha na kisha kujadiliana nao hadi wawe ni sauti zao na vibaraka mikononi mwao.

Ndani ya uhalisia huu, kumekuweko na utafiti mwingi unaoendelea kuhesabu sababu za kutelekezwa vijana na maadili yao yaliyooza. Lakini, wameikosa nukta pindi walipo pendekeza kuwa ni kutokana na kuvunjika kwa familia, au ukosefu wa elimu, au kufungiwa au dhurufu zake za kimada. Maelezo yote waliyo yataja sio sababu wala vyanzo bali zina wakilisha natija ya mateso. Chanzo msingi ni utawala wa Kimagharibi juu yao unaotumia ala za kieneo kwa sura ya serikali vibaraka mtawalia zinazo fuata amri ya Magharibi na kutabikisha njama zake.

Lakini, hata kama wanajaribu kuwatia umagharibi, licha ya hayo wangali ni vijana Waislamu ambao mtazamo wao unachipuza kutoka katika Aqeedah yao. Hivyo basi katika kura za takwimu zilizo fanywa na kikao cha Magharabi, kutokana na sampuli jumla ya vijana asilimia 79 wanakubaliana na wajibu wa kutabikisha Shari’ah kama nidhamu ya maisha huku wale wanaounga mkono vazi la kisheria la mwanamke wakiwa ni asilimia 95.

Mapinduzi ya vijana nchini Tunisia ni dalili nzuri zaidi ya kuthibitisha mwamko wao. Yalikuwa ni mapinduzi yaliyo washtua wakoloni na washirika wao, tawanya makaratasi yake na kukanganya mipango yao. Yangesambaa kote katika ulimwengu wa Kiislamu lau si kwa vibaraka hao kuwasaidia Wamagharibi kuyavuruga na kuyapoteza njia. Sasa vipi vijana watakuwa waanzilishi wa mabadiliko kama walivyo kuwa wakati wa zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)? Historia ya Kiislamu imejaa mifano yenye kuishi milele kuhusiana na vijana wanaounga mkono kadhia zao nyeti na kushiriki katika kuunda serikali. Kwa hivyo kama ambavyo kazi ya kuongoza jeshi ilipewa vijana, uzito wake kuhusiana na uwajibikaji, na uongozaji swala, uandikaji Wahyi na mamlaka ya mahakama, yanapaswa kutafutwa na wao ili leo wawe kama walivyo kuwa zamani. Mtume (saw) asema: «أوصيكم بالشباب خيراً، فإنهم أرق أفئدة... لقد بعثني الله بالحنيفية السمحة... فحالفني الشباب وخالفني الشيوخ» “Nawahusieni kuwatendea wema vijana. Kwani wao ni wenye nyoyo nyepesi mno…hakika Mwenyezi Mungu amenitumiliza kwa Al-Haneefiyah As-Samhah… Vijana wakashirikiana nami na wazee wakanipinga”.

Na yeye (saw) asema: «سبعة يظلهم الله في ظله يوم لا ظل إلا ظله إمام عادل، وشاب نشأ في عبادة الله...» “Watu aina saba Mwenyezi Mungu atawafinika na kivuli chake siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa chake yeye: kiongozi muadilifu, na kijana aliyekulia katika ibada ya Mwenyezi Mungu …”. Hivyo basi, ni muhimu kwa vijana kuwa viongozi wa dola na sio tu matineja au mabarobaro kwani umri wao unapaswa kuzingatiwa kuwa ni ule wa kufikia ukomavu unao andamana na mabadiliko ya nguvu na mabadiliko ya kiakili. Huku pia umri huu ukikadiriwa kuwakilisha mwanzo wa majukumu na huhesabiwa katika hali ambayo nguvu ya Uislamu itachanganyika na nguvu na uwezo wa umri wa ujana ili kuzalisha viongozi wakubwa na waanzilishi wa mabadiliko.

Na ili vijana wakuzwe katika ibada ya Mwenyezi Mungu, utawala wa wakoloni ni lazima ung’olewe kutoka kwa Waislamu na hilo halitatokea isipokuwa kwa kuangushwa serikali iliyo watawala juu yao. Halitatokea kupitia kubadilisha nyuso kwa nyuso nyenginezo au kupitia kubadilisha vifungu vya katiba kwa vifungu vingine vilivyo tungwa na wanadamu mithili yake. Bali litatokea pekee kwa kupitia kusimamisha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume ambayo nidhamu yake inachipuza kutokamana na Aqeedah ya Ummah huu.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هدًى]

“Sisi tunakusimulia khabari zao kwa kweli. Hakika wao walikuwa ni vijana walio muamini Mola wao Mlezi. Na Sisi tukawazidishia uwongofu” [Al-Kahf: 13].

Kwa hivyo musiwaegemee wale wanao wadhulumu na kuwatuhumu kutokuwa na uwezo, kuwa walegevu na kutokuwa na utulivu. Kama walivyokuwa wale kabla yenu – wanaume walio unda izza ya Ummah huu na hadhara yake, na kuilinda Dini hii, ardhi na heshima, nyinyi pia muna nguvu kuhusiana na Dini yenu na Ummah wenu, iliyo angazwa kupitia Aqeedah yenu, kuitikia mwito wa Dini yenu na kufanya kazi ya kuregesha maisha kamili ya Kiislamu, yatakayo rekebisha hali ya watu na kumridhisha Mola wao.

# Tushirikiane Tuokoe Vijana Kutokana na Uovu wa Itikadi ya Kisekula na Mfumo wa Kirasilimali

Hakika, ujana ni umri uliojaa nishati na ubunifu kiasi kwamba kila jamii iliyokuwa na vijana inatakiwa kujivunia nao kwani ndio kipaumbele katika kufaulisha kila nyanja ya maisha. Lakini, lakusikitisha vijana leo wanapata tabu na wanapatisha watu wengine tabu ikiwemo wazazi wao, ndugu zao, jirani zao na jamii kwa ujumla.

Kila pembe ya dunia ikiwemo Kenya tunasikia sauti za kudai mageuzi ili kuboresha hali za vijana. Mikakati, sera na sheria zikipitishwa ili kuwanusuru vijana kutokana na matatizo wanayopitia ikiwemo ukosefu wa ajira, matumizi ya mihadarati na pombe, mimba za "mapema", idadi kubwa ya maambukizi ya ukimwi, ukosefu wa maadili na heshima kwa wazee n.k.

Michakato yote hii inayofanywa na serikali za kisekula duniani ipo tu katika jaribio la kupambana na athari ya tatizo wala kattu haifichui chanzo cha matatizo wanayopitia vijana. Kabla ya kuingia kwenye kutatua tatizo ingekuwa lazima kwanza kuangalia kiini chake. Tukiangalia kwa makini tutakuta kuwa chanzo ni kuwepo kwa itikadi ya kisekula (kutenganisha dini na maisha) na mfumo wa kirasilimali ambazo chimbuko lake ni akili ya mwanadamu. Kutenganisha Dini au muongozo wake katika maisha ya wanadamu ni kuwafanya wanadamu wasimuogope Mwenyezi Mungu na sheria zake bali wawe na kila aina ya uhuru wa kufanya wanayoyataka. Kwa maana hiyo, watu wakiwemo vijana ni masekula wanaoendesha mambo yao kwa mujibu wa matamanio (uhuru) yao. Fauka ya hayo, mfumo unaowatawala wa kirasilimali upo kulinda matamanio yao na unapima vitendo vyao kwa mujibu wa maslahi na manufaa pekee! Kwa mfano kamare, mihadarati, pombe n.k licha ya kuwa na madhara katika jamii lakini kwa warasilimali ni biashara yenye faida kubwa kiuchumi. Kwa maana haya hata zile kampeni za kupambana na madawa ya kulevya n.k hayo ni danganya toto tu. Hivyo matatizo wanayopitia vijana kattu hayatarajiwi kumalizika na badala yake kila kukicha yanazidi kutokana na wao kujifunga na itikadi ya kisekula na mfumo wa kirasilimali.

Kinyume chake ni kuwa suluhisho la matatizo ya wanadamu ambao miongoni mwao ni vijana lipo ndani ya Uislamu. Kwani ni Dini ambayo chimbuko lake ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ikiwemo watu ambao miongoni mwao ni vijana. Hakika, Muumba ndiye anayestahili kupangilia viumbe namna gani viishi na sio kinyume chake. Kwa maana hiyo Uislamu ukamfunga mwanadamu na kumfanya kuwa mtumwa wa Muumba na jukumu lake ni kwenda mbio kutafuta radhi Zake kwa kujifunga na kipimo cha halali na haramu pasina kujali lawama ya anayelaumu. Uislamu umemsifu kijana kiasi kwamba akapewa nafasi miongoni mwa watu aina saba watakaopata kivuli Siku ya Kiyama. Amesimulia Abu Huraira (ra) kwamba Mtume (saw) alisema:

سَبْعَةٌ يُظِلُّهُمُ اللَّهُ فِي ظِلِّهِ يَوْمَ لاَ ظِلَّ إِلاَّ ظِلُّهُ الإِمَامُ الْعَادِلُ، وَشَابٌّ نَشَأَ فِي عِبَادَةِ رَبِّهِ

"Mwenyezi Mungu atawapa kivuli watu aina saba katika Siku ambayo hakutakuwa na kivuli isipokuwa Chake. Mtawala muadilifu, Kijana ambaye amelelewa kumuabudu Mola wake…" [Bukhari na Muslim]

Kupitia maelezo hayo ni wazi kwamba Uislamu umeweka suluhisho msingi nalo ni kwa watu jumla kujifunga na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu (swt). Kwa sababu hakuna mamlaka ya kusimamia utekelezwaji wa Uislamu kiukamilifu ndio tunashuhudia matatizo ya kila aina na watu wakitenda kila aina ya uovu kiasi kwamba ufisadi umeenea bara na baharini. Serikali zote zilizopo duniani zipo kwa ajili ya kudhamini uhuru wa watu!
Hivyo basi ni jukumu letu tushirikiane katika kukemea ulinganizi unaolenga kufanya watu wawe na utambulisho (fikra, fahamu na tabia) wa kisekula. Na wakati huo huo tupaze sauti zetu dhidi sheria zinazopitishwa ili kupigia debe Uislamu Poa bali pia kupambana na Uislamu na Waislamu kwa kisingizio cha kupambana ugaidi, itikadi kali na misimamo mikali. Muhimu zaidi tushirikiane kufanya kazi ya kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Hakika ni kupitia Khilafah kutekeleza kiukamilifu Shari'ah (Qur'an na Sunnah) ndio kutapelekea vijana na watu jumla duniani kupata utulivu, maendeleo, heshima, hadhi, cheo na ufanisi wa kweli katika maisha ya dunia na akhera. Khilafah itakuwa ndio mlinzi na ngao ya kweli kwa wanadamu wote.

**Shiriki Kampeni ya #OkoaVijana: www.facebook.com/HTKisauni**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**